# Nipashe

Alhamisi Julai 23, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0580291

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital  nipasheTZ  nipasheTZ  nipasheTZ  0745 700710

LIKE & FOLLOW US



## Watumishi waliotia nia kugombea ubunge CCM kunyimwa mshahara

UKURASA 3




UKURASA 11

# Vituko vilivyotawala kura za maoni CCM

- **Mmoja** asema ataweka pazia Mlima Kilimanjaro, mwingine azungumza Kichina akiomba kura, wabunge wakongwe wapigwa mweleka mzito...

*Endelea Ukurasa 2,3*


Steven Wasira


Pauline Gekul


Victor Mwambalaswa


Shukuru Kawambwa


Dk. Mary Nagu

Nipashe MWANGA WA JAMII

Fursa kwa Wagombea! 2020 VOTE




Gazeti la Nipashe linatoa fursa kwa wagombea wote wa vyama vya siasa kunadi sera zao kupitia kurasa zetu kwa gharama nafuu.

Wasiliana nasi
The Guardian Limited
Simu: 0686 101335,
Barua pepe: advertise@guardian.co.tz



Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

Google Play  App Store

## Magufuli aibana TAKUKURU ataka ijitazame

UKURASA 8

**MICHEZO** YANGA YAIELEKEZA MTIBWA SHIMONI UK.24  **MAONI, KATUNI** UK.6

# JPM asema siasa jukwaani ruksa

**Na Augusta Njoji, DODOMA**

RAIS John Magufuli amesema kwa sasa uwanja wa siasa uko huru baada ya Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) kutangaza ratiba yake.

Akizindua jana jengo la Ofisi ya NEC (Uchaguzi House) jijini hapa, Rais Magufuli alisema huu ndo wakati wa kujinadi na wakupiga maneno ya siasa baada ya hapo atayepatikana mshindi, kazi itaanza.

"Siasa zinabaki bungeni na kwenye halmashauri za wilaya kwa hiyo kwa sasa hivi ruksa ya ratiba itakavyokuwa imetolewa na Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi kila mmoja aende kufanya kampeni zake kwa uhuru, uwazi, akahubiri vizuri," alisema.

Rais Magufuli aliisihi tume kusimamia uchaguzi wa mwaka huu kwa kufuata Katiba, sheria na taratibu za uchaguzi zilizopo nchini.

"Navihimiza vyama vya siasa vijiepushe na vurugu katika kampeni zetu. Vurugu hazijengi, vurugu zinabomoa. Niviombe vyombo vya ulinzi na usalama visimamie usalama wa Watanzania. Yule atakayechokoza kwa kufanya fujo atakuwa amechokoza yeye, lakini mimi nina imani mambo yataenda vizuri," alisema.

"Uchaguzi huu uwe 'special' (maalum) tufanye kampeni zetu kwa upole, tufanye kampeni zetu kwa kumtanguliza Mungu. Tufanye kampeni zetu kwa kutambua sisi ni taifa Tanzania, tufanye kampeni kwa kujenga umoja wa taifa. Tunadi sera zetu na wananchi watupime kutokana na sera zetu... naamini tukienda hivyo uchaguzi utakuwa mzuri sana na utaenda vizuri sana," alisisitiza.

"Niwahakikishie mimi ni mwenzenu tunajenga nyumba moja na ni Tanzania. Nataka kuwathibitishia nitatoa ushirikiano mzuri sana kwa vyama vyote, ili tuende na maadili yetu kama tulivyofundishwa na Baba wa Taifa," alisema huku akiviomba vyama vyote vya siasa kuendesha kampeni kistaarabu.

Alibainisha kuwa Oktoba 28, mwaka huu, ambayo ni siku ya Jumatano na itakuwa ya uchaguzi mkuu, hivyo itakuwa mapumziko.

Kuhusu uhaba wa vitendea kazi kwa ofisi hiyo, alisema ataongeza Sh. milioni 500 ili kununua vifaa huku akiwataka kuleta vifaa vilivyokuwa Dar es Salaam.

Katika hatua nyingine, Rais alitoa wiki mbili kwa taasisi za umma na serikali zinazodaiwa, kuhakikisha zinalipa madeni zinayodaiwa na Shirika la Uzalishaji Mali JKT (SUMA JKT) yanayokadiriwa kufikia Sh. bilioni 11.



Rais John Magufuli akizindua jengo la ofisi za Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), akiwa na Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa na viongozi wengine katika eneo la Chikuyu B, Chamwino, mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**

# Vituko vilivyoibuka kura za maoni CCM

**Na Waandishi Wetu**

MCHAKATO wa kura za maoni kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuteuliwa kuwania nafasi za ubunge na uwakilishi katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, ulihitimishwa juzi huku kukiwa na vituko vya baadhi ya watiania kwenye majimbo mbalimbali nchini.

Miongoni mwa makada wa CCM walioibuka na vituko katika uchaguzi huo, yumo aliyetamba kuwa ataweka pazia Mlima Kilimanjaro endapo akiteuliwa kuwa Mbunge wa Moshi Mjini na kushinda katika uchaguzi huo.

**KICHINA KAWE**

Jimbo la Kawe lilikuwa limewavutia makada zaidi ya 100. Wakati wa kuomba kura kwa wajumbe, mtiania namba 75 alipopewa nafasi, aliamua kutumia lugha ya kichina na kuibua vicheko ukumbini.

Lugha hiyo ilitumika wakati kada huyo wa CCM akitoa salamu kwa wajumbe, akimnukuu Rais wa China, Xi Jinping, lakini baadaye alitoa tafsiri ya maneno hayo kwa Kiswahili akisema: "Wajibu wetu kwa wananchi ni kuwajibika kwa maneno, kwa vitendo na kwa sera, ili kutatua kero za wananchi".

Hata baada ya kujinadi kwa Kiswahili, kada huyo wa CCM ulipofika muda wa kuomba kura, alirejea kwenye lugha aliyoanza nayo ya Kichina na kuibua vicheko zaidi ukumbini.

**PAZIA MLIMA KILIMANJARO**

Katika Jimbo la Moshi mjini, mtiania Omari Mwaliko, pia aliwavunja mbavu wajumbe wa mkutano mkuu wakati akijinadi na kutamba kuwa endapo atapewa nafasi ya kuwa mbunge wa jimbo hilo, ataweka pazia Mlima Kilimanjaro.

Mwaliko ambaye alikuwa mtia nia namba 25, baada ya kusimama kuomba kura, pia alisema atalibadilii jina Wizara ya Habari endapo atapewa nafasi, uamuzi kama huo pia utafanywa kwa jina la mji wa Moshi.

"Mkinipa kura, Wizara ya Utamaduni itafufua mambo yale mnayosema uchawi, ulogaji hakuna, tutatengeneza vifaa vya kuweza kuruka angani kama wengine wanavyotengeneza," alijinadi.

Mwaliko alisema endapo atapewa kura wale wote wanaoingia ofisini na hirizi watasafishwa.

"Wanaotoa rushwa, unakuta elimu yao ni ndogo wakipewa kazi inawashinda, hiyo ni hasara, mkinipa kura mtaona hata mambo ambayo hayajawahi kutokea.

"Hata Mlima Kilimanjaro huko mbele tunaweza kuweka pazia, tutabadilisha mji kuwa wa kitakatifu, nipeni kura mpate raha," alitamba.

**SWALI LA KUUDHI**

Kwenye Jimbo la Dodoma Mjini, aliyekuwa mbunge wake kuanzia mwaka 2010 hadi 2015, Dk. David Malole, alionekana kushikwa na hasira baada ya baadhi ya wajumbe wa mkutano mkuu kumtaka awaeleze mambo aliyofanya kipindi cha uongozi wake hadi apate hamasa ya kurudi madarakani.

**SHAHADA 2 BILA AJIRA**

Katika Jimbo la Mtera, mtiania wa ubunge, Amos Hoya, aliwaomba wajumbe wamchague kwa kuwa ana elimu ya juu na anajua Kiingereza, hivyo atawatetea.

Hoya alitamba kuwa ni msomi na ana shahada mbili ambazo amezipata India, lakini licha ya kuwa msomi wa ngazi ya juu, amekuwa akihangaika kupata ajira, hivyo kuna haja kuwatumikia wananchi kupitia ubunge.

"Mimi ni msomi, nimesoma nchini India. Nimezunguka kutafuta ajira sijapata, ninaomba mnichague nitawatumikia," alisema na kusisitiza kuwa kama watamchagua, atawatetea kwa kuzungumza Kiingereza sehemu mbalimbali na kuipa heshima Mtera kwamba ina wasomi.

"Ninaongea Kiingereza kwa ufasaha, nitawatetea kila mahali, ila mpaka umri huu sina ajira, lakini nimesomea siasa chuo, hivyo ninaijua vizuri," alitamba Hoya aliyekuwa amevaa miwani, huku mikono ikiwa mfukoni.

**KISUKUMA KWA WAGOGO**

Katika jimbo hilo hilo, mtiania Mazari Omari, alisema kwamba yeye ni Msukuma aliyezaliwa Nzega, lakini kwa muda mrefu amekuwa akiishi Dodoma na ana watoto watano.

Huku akizungumza kwa Kisukuma, kada huyo wa CCM alisema uwezo anao na atawasaidia wafugaji kwa kuwa ana kiwanda cha nyama.

**'NIACHIE NA MKE WANGU'**

Mbunge aliyemaliza muda wake katika jimbo hilo, Livingstone Lusinde, akiomba kura kwa wajumbe, alisema anajua amefanya mambo mengi katika jimbo hilo, lakini kama kuna mambo mabaya aachiwe yeye na mke wake.

"Wakati ninaingia madarakani, umeme ulikuwa katika vijiji viwili, leo kuna umeme katika vijiji 30, nimetoa hela zangu mfukoni zaidi ya Sh. milioni 82 kwa ajili ya kugharamia maziko, niacheni niendelee kuwatumikia," alisema.

**BAISKELI KILA KATA**

Katika Jimbo la Masasi, mtiania Emmanuel Milanzi, alisema iwapo CCM ikimpa ridhaa ya kugombea jimbo hilo na kushinda, atatoa baiskeli katika kila ofisi ya kata ya chama hicho, ili kurahisisha utendaji kazi kwenye maeneo hayo.

Alisema kuwa, baadhi ya watendaji wa ofisi za kata 14 za jimbo hilo wamekuwa wakifanya kazi katika mazingira magumu ikiwamo kutembea kwa miguu, jambo ambalo limekuwa kikwazo katika utendaji wao.

**SHIKAMOO**

Aliyekuwa Mbunge wa Muheza, Balozi Adadi Rajabu, amefanikiwa kuuona mwanga wa kutetea kiti chake baada ya kuongoza katika kura hizo za maoni.

Hata hivyo, haikuwa rahisi kwa Mkurugenzi huyo wa zamani wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) kuongoza katika mchakato huo. Balozi Adadi wakati anaomba kura kwa wajumbe wa mkutano mkuu Wilaya ya Muheza, alilazimika kuwasalimu kwa kuwaamkia "shikamoo".

## HABARI KITAIFA

# Wabunge wakongwe waanguka CCM

Na Romana Mallya

MCHAKATO wa kura za maoni kuomba ridhaa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuteuliwa kuwania nafasi za ubunge na uwakilishi katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu, ulihitimishwa juzi huku wabunge wakongwe wa chama hicho wakianguka.

Majimbo 16 ya watia nia wakongwe waliorusha ndoano zao kwa mara nyingine kwa nia ya kutetea nafasi zao, yameshuhudiwa kuwa na sura mpya.

Miongoni mwa majimbo hayo ni Kyela ambalo kwa muda wa miaka 15 lilikuwa likishikiliwa na Dk. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo. Katika mchakato wa kura za maoni jimboni humo, Dk. Mwakyembe ameangushwa na Ally Jumbe 'Kinanasi'.

Profesa Jumanne Maghembe, aliyekuwa Mbunge wa Mwanga mkoani Kilimanjaro kwa miaka 15, ameshindwa baada ya kupata kura 130 dhidi ya kinara Anania Thadayo aliyepata kura 176.

Jimbo la Handeni Vijijini mkoani Tanga lililoongozwa na Mboni Mhita kwa miaka mitano, lilikuwa na ushindani mkali na mwakilishi huyo wa jimbo ameshika nafasi ya pili kwa kupata kura 136 dhidi ya kinara Charles Sungura aliyepigiwa kura 168.

George Lubeleje, aliyekuwa Mbunge wa Mpwapwa mkoani Dodoma, aliangushwa mwaka 2010 kisha akarudi 2015, lakini safari hii kwenye kura za maoni ameshika nafasi ya tano kwa kupata kura 10, huku aliyeongoza, George Malima, akipata kura 263.

Katika Jimbo la Ulanga, aliyekuwa mbunge wake, Goodluck Mlinga, akiliwakilisha kwa vipindi viwili, ameshika nafasi ya pili kwa kura 123 dhidi ya kinara Salim Hashimu aliyejinyakulia kura 219.

Dk. Shukuru Kawambwa, aliyehudumu kwa vipindi vitatu kuanzia 2005 katika Jimbo la Bagamoyo, amepata kura 90 huku kinara akiwa ni Muharami Mkenge aliyeongoza kwa kupigiwa kura 157.

Jimbo la Tunduru Kaskazini, ambalo lilishikiliwa na Ramo Makani tangu mwaka 2010, limeshuhudiwa pia Naibu Waziri huyo wa zamani wa Maliasili na Utalii, akianguka.

Wabunge wengine wakongwe walioanguka ni pamoja na Gerson Lwenge, aliyekuwa Mbunge wa Wanging'ombe mkoani Njombe, ambaye amepata kura 159, akiangushwa na Enock Kiswaga, aliyepata kura 175.

Venance Mwamoto, aliyekuwa Mbunge wa Kilolo mkoani Iringa, ameangushwa na Jastin Nyamoga, aliyekuwa Mbunge wa Mvomero, Suleiman Sadiq, amezidiwa kete na Amos Makala, aliyekuwa Mbunge wa Igunga, Dk. Dalaly Kafumu, ameshika nafasi ya tatu kwa kura 57 huku kinara akiwa ni Henry Kabeho aliyepigiwa kura 202.

Katika Jimbo la Lupa, lililokuwa likiwakilishwa na Victor Mwambalaswa kwenye Bunge lililopita, kumeshuhudiwa akianguka katika kura za maoni baada ya kuambulia kura 86 dhidi ya 476 za kinara Masache Kasaka.

Wengine walioanguka majimboni ni Murtaz Mangungu, aliyekuwa Mbunge wa Kilwa Kaskazini na Ezekiel Maige, aliyekuwa Mbunge wa Msalala.



Jaji Kiongozi wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Dk. Eliezer Feleshi (kushoto), akizungumza na watendaji wa mahakama za mkoa wa Tanga, alipotembelea kukagua ujenzi wa jengo jipya la Mahakama ya Wilaya ya Kilindi, jana. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

# Hazina yaagiza waliotia nia kutolipwa mshahara

Na Elizabeth Zaya

OFISI ya Msajili wa Hazina, imewataka wakurugenzi wote wa halmashauri na taasisi zote za serikali kutowalipa mshahara wa Julai watumishi wake wote waliochukua fomu ya kugombea nafasi ya uongozi wa kisiasa kupitia vyama vya siasa.

Barua iliyoandikwa Julai 21, mwaka huu na Msajili wa Hazina, Neema Msonda, ambayo imesambaswa katika taasisi za serikali, imewataka pia wakurugenzi na wakuu wa taasisi hizo kuandaa na kuwasilisha katika ofisi ya Msajili wa Hazina, taarifa ya utekelezaji wa maelekezo hayo kabla au ifikapo Julai 25.

"Tunawafahamisha kuwa mnatakiwa kutowalipa mshahara wa mwezi Julai, 2020, watumishi wote wa umma waliochukua fomu na kugombea nafasi ya uongozi wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa katika mchakato wa uchaguzi unaoendelea kutoka katika taasisi unayoisimamia," ilieleza taarifa hiyo na kuongeza:

"Maelekezo haya ya kutolipa mshahara wa mwezi Julai, yanawahusu watumishi waliopatiwa vibali/ruhusa na waajiri wao pamoja na watumishi waliogombea bila vibali kutoka kwa waajiri wao au kupitia mamlaka stahiki." Kutokana na maelekezo hayo ya Msajili wa Hazina, baadhi ya taasisi za serikali kikiwamo Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere, ni miongoni mwa taasisi ambazo zimeanza kutekeleza maelekezo hayo.

Chuo hicho jana kiliwaandikia barua watumishi wake waliotia nia na kuchukua fomu za kugombea nafasi za uongozi huo wa kisiasa.

"Napenda kuwajulisha kuwa tumepata maelekezo ya kuwasimamishia mshahara wa mwezi Julai, 2020 watumishi wote waliochukua fomu za kugombea nafasi za uongozi wa kisiasa kupitia chama chochote cha siasa katika mchakato wa uchaguzi unaoendelea," ilieleza barua ya Mkuu wa chuo hicho, Dk. Godwin Kaganda.

"Hivyo, watumishi wote waliochukua fomu za kugombea mnatakiwa muwasilishe majina yenu kwenye ofisi ya utumishi utawala na rasilimali watu kabla ya saa tisa alasiri leo (jana), mtumishi atakayekiuka agizo hili atachukuliwa hatua za kinidhamu kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu za utumishi wa umma."

**THRDC YAWAFUKUZA WANACHAMA WAKE 11**

Wakati hayo yakitokea kwa taasisi za serikali, Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu (THRDC), nao umewafukuza kazi wanachama wake 11 waliokwenda kugombea bila kufuata kanuni na taratibu za mtandao huo za kwenda kugombea.

Mratibu wa kitaifa wa THRDC, Onesmo Ole Ngurumo, alisema watumishi hao walisimamishwa kuanzia Julai 23 hadi pale watakapopeleka utetezi wa kwa nini wasifutwe kabisa uanachama kwa kushiriki uchaguzi huku wakiwa bado ni wanachama wa mtandao huo.

## Waliounga mkono 'juhudi' waanguka kura za maoni CCM

Na Waandishi Wetu

MAKADA wa vyama vya upinzani waliojiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kutaka kutetea nafasi ya ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka huu, wamefanya vibaya kwenye kura za maoni za chama hicho.

Katika kura hizo zilizoanza juzi na kuhitimishwa jana, kumeshuhudiwa pia baadhi ya makada wakongwe wa CCM na mawaziri wakianguka.

Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Godwin Mollel, ni miongoni mwa makada wapya wawili wa CCM walioona mwanga wa kutetea majimbo yao kati ya waliokuwa wabunge wa Bunge la 11 wakitoka upinzani na kujiunga na chama tawala.

Dk. Mollel alimshinda kwa kura moja aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Tabora, Aggrey Mwanri, katika kinyang'anyiro cha kusaka kuteuliwa kuwania Jimbo la Siha mkoani Kilimanjaro.

Mbali na Dk. Mollel, mwingine ni aliyekuwa Mbunge wa Ukerewe, Joseph Mkundi ambaye miaka miwili iliyopita, alijivua uanachama na nyadhifa zake zote ndani ya CHADEMA na kuhamia CCM.

**TANDAHIMBA**

Aliyekuwa Mbunge wa Tandahimba kupitia Chama cha Wananchi (CUF) na baadaye kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM), Katani Katani, ameshika nafasi ya pili akipigiwa kura 308 dhidi ya kura 324 za Dk. Twahili Salum.

Wakati hali ikiwa hivyo kwa makada hao wapya wa CCM, mkoani Mbeya, mkoani Morogoro, aliyekuwa Mbunge wa Kilombero kupitia CHADEMA na baadaye mwaka huu kujiunga na CCM, Peter Lijualikali, ameanguka pia kwenye mchakato huo sawa na aliyekuwa Mbunge wa Liwale kupitia CUF na baadaye kujiunga na CCM, Zuberi Kuchauka.

Kanda ya Kaskazini, makada wapya watano wa CCM katika mikoa ya kanda hiyo wakiwamo wabunge na Meya wa Jiji la Arusha, wameangukia pua katika kura hizo za maoni.

Katika mkutano mkuu maalum wa uchaguzi uliofanyika Julai 20 na 21 mwaka huu katika maeneo mbalimbali, waliokuwa wabunge wa majimbo ya Arumeru Mashariki, Monduli, Simanjiro na Babati Mjini na Meya wa zamani wa Jiji la Arusha waliojiuzulu nyadhifa zao na kuunga mkono juhudi, wametoswa na wapigakura.

Joshua Nassari, aliyekuwa Mbunge wa Arumeru Mashariki (CHADEMA) kabla ya kutimkia CCM, aliambulia nafasi ya nne katika kura za maoni, wakati aliyekuwa Mbunge wa Babati Mjini (CHADEMA) kabla ya kutimkia CCM na kuchaguliwa tena kuliongoza jimbo hilo, Pauline Gekul, amepoteza nafasi yake katika mchakato huo.

Vilevile, aliyekuwa Mbunge wa Monduli (CHADEMA) na baadaye kuendelea na wadhifa huo akiwa CCM, Julius Kalanga, naye ameanguka katika mchakato wa kura za maoni za kumpata mgombea atakayepeperusha bendera ya chama tawala. Mwingine ni James Ole Millya wa Simanjiro ambaye aliliwakilisha jimbo hilo kwa vipindi viwili tofauti akiwa CHADEMA na baadaye CCM. Yumo pia aliyekuwa Meya wa Jiji la Arusha (CHADEMA), Calist Lazaro ambaye alijiuzulu wadhifa huo na kujiunga na CCM.

# Umakini watakiwa mitandao ya jamii

**Na Mwandishi Wetu**

KUNA haja ya kuchukua hatua madhubuti kukuza na kuwezesha amani hasa katika kipindi hiki ambacho mitandao ya kijamii inatumika kueneza uchochezi, Mkurugenzi wa Global Peace Foundation (GPLC) Tanzania amesema.

Martha Nghambi amesema mitandao ya kijami inaweza kutumika kuzuia mizozo na uenezi wa msimamo mkali na pia kukuza uelewa na uvumilivu.

"Lazima tuchukue hatua kuhakikisha tunapanda mbegu za amani na uvumilivu kwa kila mmoja, na mitandao ya kijamii ni jukwaa zuri la kufikia vijana," alisema Nghambi alipozungumza na waandishi wa habari jana.

Alisema GPLC itafanya mkutano wa mtandaoni Julai 30 hadi 31 mwaka huu kujadili mbinu mbalimbali za kukuza amani.

"Mkutano huo ulipangwa kufanyiwa Nairobi, Kenya lakini kwa vile nchi nyingi bado zinaendelea kuchukua tahadhari dhidi ya Covid-19, mkutano utafanywa mtandaoni," alisema.

Alisema mkutano huo unafuatia mkutano wa mwisho uliofanyika Uganda na chini ya usimamizi wa mgeni rasmi Rais Yoweri Museveni, ukikusanya zaidi ya wajumbe 1,000 wakiwamo viongozi mbalimbali.

Katika mkutano huo, hotuba ya Rais wa Kenya, Uhuru Kenyatta, ilisomwa na Katibu wa Baraza la Mawaziri, Eugene Wamalwa na ya Rais wa Tanzania, John Magufuli, ilisomwa na aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria, Balozi Dk. Augustine Mahiga.

Nghambi alisisitiza umuhimu wa ushiriki wa vijana kama wanufaika wa moja kwa moja wa taasisi hiyo.

"Kuwashirikisha vijana kunawafanya kuwa watetezi na pia inawapa nguvu kuchukua hatua badala ya kutumiwa kuwa wachochezi.

"Tunao mradi unaoendelea unaoitwa 'Wanawake Sasa', ambao unalenga kuwezesha wanawake vijana katika uongozi bora, kuzuia migogoro, kukuza amani kabla ya na baada ya uchaguzi," alisema. GPLC ni jukwaa linalokusanya viongozi kutoka serikalini, wafanyabiashara, wasomi, mashirika yasiyo ya kiserikali na taasisi za kidini, kubadilishana mitazamo juu ya uongozi bora katika jamii.

GPLC mwaka huu itabainisha uzoefu wa Kenya kulinda ustawi wa amani kwenye pembe ya Afrika ikiwamo juhudi zake kusimamia utulivu wa amani Somali, Sudani na Sudani Kusini.

# Waandishi wa habari washauriwa kusoma

**Na Enock Charles**

WAANDISHI wa habari wametakiwa kusoma zaidi vitabu na utafiti mbalimbali, ili kuwa na uwezo mkubwa wa kuandika taarifa kwa kina zilizo bora badala ya kujikita katika kuandika habari za matukio. Akizungumza jana jijini Dar es Salaam jana wakati wa uzinduzi wa ripoti ya hali ya vyombo vya habari kwa mwaka 2019, Mwandishi Mkongwe wa habari nchini, Jenerali Ulimwengu, alisema kwenye kusoma ndiko kuna maarifa ya kuongeza uwezo wa kuchambua mambo.

Ripoti hiyo iliandaliwa kwa ushirikiano kati ya Shule Kuu ya Uandishi wa Habari na Mawasiliano wa Umma (SJMC) katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Ubalozi wa Uswisi.

Aidha, aliwataka waandishi kuwekeza katika kusoma na kutambua kuwa wana wajibu mkubwa wa kuandika taarifa zilizokamilika na zenye manufaa kwa jamii na Taifa kwa ujumla.

"Kazi ya kuandika ni kazi ya mwisho kabisa kwa mwandishi wa habari, kazi ya kwanza ya mwandishi wa habari ni kusoma... ni muhimu kutambua kuwa miongoni mwa watu katika jamii unayoiandikia wapo wenye taarifa zaidi ya jambo unaloliandikia kuliko wewe," alibainisha Jenerali Ulimwengu.

Alisema kutokana na kutokusoma, kuna ombwe kubwa la uandishi mzuri wa habari hasa kwa miaka ya hivi karibuni, jambo ambalo limedhihirishwa katika ripoti ya utafiti wa ubora wa maudhui katika vyombo vya habari nchini.

Akizungumza wakati wa kuzindua ripoti hiyo, Mhadhiri wa SJMC, Abdallah Katunzi, alisema katika ripoti mwaka 2019 imeonyesha kuwa asilimia 40 ya taarifa katika vyombo vya habari hazikuwa na mtazamo, huku asilimia 18 zikiwa ni za mtazamo mmoja .

Alisema utafiti huo pia ulibaini vyombo vya habari kuwa na vyanzo vichache kwa kutolea mfano kuwa asilimia 66 ya habari kwa mwaka 2019 hazikuwa na chanzo kilichotokana na mwanamke/wanawake na asilimia 22 ya habari zikiwa na chanzo kimoja kutoka kundi la wanawake na asilimia 12 tu zilizokuwa na chanzo cha kutoka kwa wanawake wawili au zaidi.

"Tatizo la habari za kuwa na chanzo kimoja au mtazamo mmoja limeongezeka kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na mwaka 2018, vyombo vyote vya habari (radio, luninga na magazeti) vimetumia vyanzo vichache zaidi," alisema Katunzi.

Naye, Katibu wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Neville Meena, akichangia mjadala kuhusiana na ripoti hiyo, aliviomba vyombo vya habari kutokuogopa kukosoa pale inapobidi kwa kuwa ni wajibu wa msingi wa vyombo vya habari, na kwamba italeta mabadiliko chanya katika nyanja za kiuchumi, kisiasa na kijamii.




Mtafiti wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Abdallah Katunzi, akizungumza jijini Dar es Salaam jana, na wahariri wa vyombo mbalimbali vya habari jana, baada ya kuzinduliwa kwa ripoti ya ubora wa maudhui ya vyombo hivyo, nchini kwa mwaka 2019. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Zungu atamba Mchuchuma itaondoa uhaba wa malighafi

**Na Mwandishi Wetu,** KIBAHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Mussa Azzan Zungu, amesema utatuzi wa kweli wa upatikanaji wa malighafi kwa viwanda vya chuma nchini utatokana na kuanza kazi kwa mradi wa Mchuchuma katika Wilaya ya Ludewa, Mkoa wa Njombe.

Akizungumza na baada ya kukagua na kuelezwa na viongozi wa kiwanda cha nondo cha Hong yu Steels (T) Co, Ltd kilichopo Kibaha, mkoani Pwani kwamba kiwanda chao kimesimamisha uzalishaji kutokana na ukosefu wa malighafi, Waziri Zungu alisema uhaba wa malighafi utakwisha baada ya Mradi wa Mchuchuma kuanza kufanya kazi. "Serikali inatambua uhaba wa malighafi uliopo hususani katika viwanda vya chuma na inaendelea kuchukua hatua ili kukamilisha mradi wa Mchuchuma ambao utaleta suluhisho la kudumu, na kuondoa uhaba wa malighafi inayolalamikiwa. Uhaba huo ukiisha, kasi ya ukuaji wa sekta ya viwanda hapa nchini itaongezeka," alisema waziri.

Alisema kwa sasa viwanda vingi nchini vinategemea vyuma chakavu kama malighafi, na kwamba jambo hilo linachochea uharibifu wa miundombinu kama madaraja, reli na nyaya za umeme na simu. "Kukosekana kwa malighafi ya uhakika kwa viwanda vinavyotegemea vyuma chakavu kama malighafi kumesababisha kuhujumiwa kwa miundombinu iliyotengenezwa kwa gharama kubwa na serikali," alisema na kuendelea:

"Zipo taratibu za kufuata katika kukusanya, kusafirisha na kuhifadhi vyuma chakavu. Naendelea kusisitiza, Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira kuwachukulia hatua za kisheria wakusanyaji na wasafirishaji wa vyuma chakavu wasiofuata taratibu na kanuni zilizowekwa katika ufanyaji wa biashara ya vyuma chakavu."

Waziri alikihakikishia kiwanda hicho kwamba kitapata mzigo wa malighafi uliokwama kati ya Tanzania na Malawi baada ya taratibu za uingizaji malighafi ya aina hiyo kukamilika.

"Ipo mikataba ya kimataifa ambayo kama nchi tumeridhia na lazima iheshimiwe. Hata hivyo tutakaa na timu ya wataalamu na kuangalia ni namna gani tunatatua changamoto ya malighafi hiyo kuingia nchini ili kiwanda kiendelee na uzalishaji, kutengeneza ajira kwa vijana na kuchangia ukuaji wa pato la taifa," alisema.

Meneja wa NEMC Kanda ya Mashariki, Arnold Mapinduzi, alisema watawachukulia hatua wafanyabiashara wa vyuma chakavu ambao wanakiuka utaratibu uliowekwa bila kujali rangi wala cheo cha mhusika. "Wafanyabiashara wa vyuma chakavu wanatakiwa kufuata taratibu ikiwemo ujazaji wa fomu ya ukusanyaji vyuma chakavu ili NEMC ijiridhishe wapi malighafi hiyo imepatikana, hali ambayo inasaidia katika utunzanji wa miundombinu. Tutawachukulia hatua kama ambavyo waziri alivyoagiza kwa mujibu wa sheria zilizopo," alisema Mapinduzi.

HABARI KITAIFA

# Wanahabari waliojitosa sasa ubunge watakiwa kuondoka kwenye fani

**Na Mwandishi Wetu**

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limesema kuwa waandishi waliojitokeza kuchukua fomu za kugombea nafasi mbalimbali za kisiasa ni haki yao ya msingi kama walivyo raia wengine hapa nchini, lakini wanapaswa kuondoka katika uandishi wa habari.

Katibu Mtendaji wa MCT, Kajubi Mukajanga, aliyasema hayo wakati wa mahojiano na waandishi wa habari katika ofisi za baraza hilo jana na kuongeza kwamba mwandishi wa habari kama sehemu ya jamii ana haki ya kuwa mpiga kura na pia ana haki ya kuwa mpigiwa kura.

"Hilo halina mjadala inatakiwa aondoke kwa sababu hakuna namna ambayo tutaendelea kumwamini wakati yeye amevaa shati la kijani, au la zambarau, au la bluu na anapiga sera za chama, haiwezekani akaendelea kuwa ndani ya chumba cha habari," alisisitiza. Alisema waandishi wa habari wanapaswa kuliheshimu hili, lakini viongozi wa vyumba vya habari na wamiliki wa vyombo vya habari wanapaswa kulisisitiza na kulitolea miongozo iliyo wazi ndani ya vyumba vya habari. "Sisi tunavyoona ni kwamba, ikimpendeza mtu kwenda kwenye siasa, aende kwenye siasa moja kwa moja, akitaka baada ya hapo kujihusisha na kazi ya uandishi wa habari, ingependeza isiwe ndani ya chombo cha habari, kwa sababu watu wataendelea kumtazama kama mgombea, kama kada."

Alifafanua kuwa mwandishi wa habari ambaye amejihusisha na siasa za ushindani, anaweza kuwa mwana safu (Columnist), lakini chini ya safu yake ielezwe wazi kuwa huyu ni mwandishi wa siku nyingi na aliwahi kugombea kupitia chama fulani cha siasa.

Hii itasaidia hata mtu atakayeisoma safu yake au maoni yake aweze kujua mtu huyu anatokea wapi, na ana msimamo gani, hilo ni jambo la muhimu ambalo kila chombo cha habari ni lazima kikaweka utaratibu wake.

Akizungumzia kuhusu chombo cha habari kuwa na msimamo na chama fulani, alisema si dhambi hata kidogo, na kuongeza kuwa katika historia ya vyombo vya habari hasa vya magazeti wakati yanaanzishwa huko Ulaya, yalikuwa yanaanzishwa yakiwa ya kutetea hoja za vyama vya siasa.

"Chombo cha habari kinaanzishwa na kinajulikana kwamba hiki ni cha mlengo wa kushoto, au cha sera za labour, hiki ni cha mlengo wa kulia, kinasimamia sera za conservative ndivyo vilivyoanzishwa," alifafanua.

Aliwakumbusha waandishi wa habari kuwa kazi ya uandishi wa habari inamtaka mwandishi wa habari aonyeshe kwamba anaweza kutenda haki wakati wa uchaguzi kwa maana asipendelee upande wowote, wala usiuminye upande mwingine kwa faida ya upande unaoupenda yeye.

Alivitaka vyombo vya habari vyenye lengo la kuonyesha mapenzi kwa chama fulani, kuweka wazi nia hiyo, lakini visigeuke kuwa vyombo vya propaganda kwa maana visiseme uongo, na badala yake viendelee kutoa haki sawa, visikandamize upande mmoja na visinyime upande mwingine haki ya kusikika, visiseme uongo, visipakazie upande mwingine kwa manufaa ya upande wake na visichanganye maoni ndani ya habari kwa manufaa ya chama chao.

Alisema waandishi wa habari wajitahidi kubaki kuwa wanahabari. "Mimi ningependa hii tasnia iwe na heshima, na iheshimiwe, ni kazi yenye majukumu makubwa, na ningependa waandishi wa habari wazuri wajitahidi kubaki katika taaluma hii," alisema Kajubi. Aliwaasa waandishi wa habari kutenganisha mapenzi ya kisiasa, ushabiki, na uandishi wa habari.

"Taaluma ibaki kuwa taaluma, na wanaotaka kwenda kwenye siasa, hawakatazwi waende kwenye siasa, na wafanye hivyo mapema, na wafanye hivyo kila mtu ajue, na wasiendelee kukaa ndani ya vyombo vya habari, au kukaa na vyeo vya kusimamia waandishi wa habari wakati wao tayari ni makada walioingia katika siasa za ushindani," alisisitiza.

# Jafo aagiza halmashauri zitumie bidhaa za ndani

**Na Gwamaka Alipipi**

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais - Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jafo, ameziagiza halmashauri zote kuhakikisha wanatumia bidhaa zinazozalishwa na viwanda vya ndani katika ujenzi wa miradi ya maendeleo wanayoitekeleza ikiwamo ya shule, masoko na hospitali.

Alitoa agizo hilo jana jijini Dar es Salaam alipotembelea kiwanda kinachozalisha vifaa vya umeme vya Kilimanjaro Cables (AFRICAB) na kueleza kuwa matumizi ya bidhaa zinazozalishwa nchini, zikiwamo bidhaa za umeme, ni muhimu kutumika katika miradi ya serikali kutokana na ubora wake.

"Hakuna shaka kwamba hivi sasa viwanda vyetu, kikiwamo hiki cha AFRICAB, vinafanya kazi nzuri na kubwa katika kusukuma mbele maendeleo ya nchi yetu, ambayo kwa sasa imeingia katika uchumi wa kati, nitoe rai kwa halmashauri zote kuhakikisha zinaunga mkono juhudi hizo kwa kununua bidhaa zinazozalishwa na viwanda vyetu," alisema.

Waziri Jafo alisema matumizi ya bidhaa zinazozalishwa nchini, mbali na kuzingatia ubora, pia zinasaidia katika kulinda fedha ya ndani ambazo zingetumika kuagiza bidhaa kutoka nje ya nchi.

Alikipongeza kiwanda hicho kwa hatua mbalimbali za utengenezaji wa bidhaa za umeme zikiwamo nyaya, mabomba (PVC) soketi pamoja na transfoma, huku akisisitiza kuwa hatua hiyo imeonyesha kwa dhati juhudi za Tanzania katika harakati za kukuza viwanda kama ilivyosisitizwa kwa nyakati tofauti na Rais John Magufuli.

"Haya ni maendeleo makubwa kwa taifa letu, tunapaswa kujisifia kwa hatua hii, kikubwa endeleeni kuzalisha bidhaa bora na zenye kukidhi matakwa ya taifa letu, huu ndiyo uzalendo wa kweli," alisema Waziri Jafo.

Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Godwin Gondwe, mbali na kukipongeza kiwanda hicho kwa juhudi za kuunga mkono serikali ya ujenzi wa viwanda, alisema ofisi yake itahakikisha inayatekeleza maagizo ya Waziri Jafo kwa kuhakikisha ujenzi wa miradi yote ya serikali katika wilaya hiyo inatumia bidhaa zinazozalishwa na kiwanda hicho na vingine vilivyopo nchini.


**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**

**TAARIFA KWA UMMA:**

**USAJILI NA MAOMBI YA LESENI NA VITAMBULISHO KWA WAONGOZA WATALII "TOUR GUIDES" NCHINI KWA MWAKA 2020**

Wizara inaujulisha Umma pamoja na Wafanyabiashara za utalii nchini kuwa, maombi ya usajili wa Leseni za Biashara za Utalii (TTBL) kwa Waongoza watalii **(Tour Guides)** pamoja na vitambulisho kwa mwaka 2020 yameanza kupokelewa rasmi kwa njia ya mtandao. Unakumbushwa kufanya maombi ndani ya siku 30 kuanzia tarehe ya tangazo hili. Hatua hii ni kuwezesha upatikanaji kwa wakati wa leseni husika ambayo hutolewa kwa mujibu wa kifungu cha 21 cha Sheria ya Utalii Na. 29 ya mwaka 2008 na kifungu cha 3(2) cha kanuni ya Waongoza Watalii.

Hivyo, upokeaji wa maombi yote ya usajili wa leseni kwa Waongoza Watalii Pamoja na vitambulisho unafanyika kupitia mfumo mpya wa kielektroniki wa Wizara, ***MNRT – Portal,*** unaopatikana katika tovuti ya Wizara kwa kiunganishi **portal.maliasili.go.tz**. **Izingatiwe kuwa,** ni kosa kisheria kuwasilisha taarifa za uongo na adhabu yake ni pamoja na kufutiwa leseni.

Kwa maelezo zaidi tafadhali tembelea tovuti yetu ***www.maliasili.go.tz*** au fika kwenye Ofisi zetu za Makao Makuu zilizopo UDOM, Dodoma au Ofisi za Utalii za Kanda zilizopo Jengo la Mpingo - Dar es Salaam; PSSSF - Mwanza; Jengo la NSSF - Iringa; na TANAPA Makao Makuu - Arusha.

**Imetolewa na:**
**MKURUGENZI WA UTALII**
**WIZARA YA MALIASILI NA UTALII**
**S. L. P 1351**
**40472 DODOMA**
**Simu: +255 712721932**
**Barua pepe: dt@maliasili.go.tz**
**13 Julai, 2020**

215821702

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uchaguzi kutofanyika Jumapili kutaongeza ushiriki wapigakura

**TUME** ya Taifa ya Uchaguzi (NEC) imetangaza kwamba uchaguzi mkuu wa urais, ubunge na udiwani utafanyika Jumatano badala ya Jumapili kama ilivyozoeleka.

Hayo yalibainishwa juzi jijini Dar es Salaam na Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi, (NEC), Jaji wa Rufani mstaafu, Semistocles Kaijage, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari, na kuongeza kuwa uchaguzi mkuu wa mwaka huu unatarajia kufanyika Oktoba 28.

Pia Jaji Kaijage alieleza kuwa alisema Agosti 25, kutafanyika uteuzi wa wagombea kiti cha urais, makamu wa rais, ubunge na udiwani na Agosti 26 kampeni za uchaguzi zitaanza hadi Oktoba 27.

Ingawa Jaji Kaijage, hakutoa ufafanuzi kuhusiana na uamuzi wa uchaguzi mkuu kufanyika Jumatano, lakini kumekuwapo na mapendekezo kutoka kwa wadau wa uchaguzi na makundi mengine ya jamii nchini kutaka uchaguzi huo kutofanyika Jumapili kama ilivyokuwa kwa miaka yote.

Wamekuwa wakisema kuwa watu wengi wamekuwa wakipata wakati mgumu kwenda kupiga kura Jumapili sambamba na kuhudhuria ibada makanisani.

Hoja zilizokuwa zinatolewa zina mashiko, kwa kuwa kimsingi, watu ambao hufanya ibada siku ya Jumapili wanakuwa katika wakati mgumu wa kutekeleza majukumu mawili kwa siku moja.

Kwenda kwenye ibada ni jukumu muhimu kwao kwa kutilia maanani kuwa suala la kuabudu ni haki ya msingi ya kila raia kwa mujibu wa katiba ya nchi.

Aidha, kushiriki katika uchaguzi wa kuchagua viongozi ni jukumu la kila mmoja mwenye sifa za kupiga kura, hivyo ni majukumu ambayo kutekelezwa pamoja kwa siku moja, kunakuwapo na ugumu.

Baadhi ya watu wenye jukumu la kwenda kwenye ibada makanisani huanza shughuli za kuabudu kuanzia mapema asubuhi hadi mchana, hivyo kwa mazingira hayo inawawia vigumu kutoka na kwenda kwenye vituo vya kupigia kura kuwachagua viongozi wanaowataka.

Kwa upande mwingine, sio rahisi kuamkia katika vituo vya kupiga kura kisha kwenda kwenye shughuli za ibada kwa kuwa mara nyingi wakati wa asubuhi vituo vinapofunguliwa kunakuwa na misururu ya wapigakura.

Kutokana na hali hiyo, inamlazimisha mhusika kutekeleza jukumu moja aidha kwenda kuabudu au kutumia siku hiyo kwa ajili ya kutekeleza wajibu wa kuwachagua viongozi.

Uamuzi wa huu wa uchaguzi mkuu kutofanyika Jumapili ni mzuri na utaboresha mazingira ya ushiriki wa wapigakura wengi, hivyo kuondoa tatizo lililokuwa likilalamikiwa la wapigakura wengi kujiandikisha, lakini siku ya uchaguzi kujitokeza wachache. Suala la kujitokeza wapigakura wachache siku ya uchaguzi limekuwa likionekana kuwa ni tatizo, kiasi cha kuzua mjadala kwa wadau wa uchaguzi na makundi mengine katika jamii nchini.

Wako ambao wamekuwa wakipendekeza kuwa suala hilo litazamwe kwa upana kisha kupatiwa ufumbuzi wa kudumu. Hata hivyo, kwa uamuzi wa kubadili siku ya kupiga kura tunauona kuwa ni moja ya jitihada nzuri zilizofanywa na serikali.


Baadhi ya nchi za Afrika, zikiwamo za jirani zilishaanzisha utaratibu wa kufanya uchaguzi mkuu siku ambazo sio Jumapili, pengine baada ya kuona kuwa siku hiyo inawakosesha fursa wapigakura wengi kushiriki.

Tunaamini kuwa vikwazo vingine ambavyo vinakwaza wapigakura wengi kujitokeza kuendelea kutafutiwa ufumbuzi, lengo likiwa kuwapa fursa Watanzania wengi kushiriki kuchagua viongozi wanaowataka.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:

**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Yasmine Protace

# Utapeli mpya wa simu; mzazi au mtoto amezidiwa shuleni

**HADI** sasa kuna maendeleo makubwa katika manufaa yatokanayo na matumizi ya simu nchini, tukiungana na dunia ilivyo.

Pia, kuna sura nyingine ambayo ni mbaya, kuwapo matukio ya utapeli kupitia mitandao ya simu inayoendelea katika maeneo mbalimbali, watu kuibiwa pesa, wanaporubuniwa kupitia mifumo yao hiyo ya kimtandao.

Mtindo wanaotumia matapeli hao ni matumizi ya ujumbe mfupi wa simu wakijaribu kumrubuni mtu anayefanya biashara na hata kutoa wazo la kunufaika kiuchumi.

Watu mara nyingi wanaangukia kurubunika, hasa kutokana na uhalisia wa hali duni ya kiuchumi, hata kuhamasika huenda akajinusuru kiuchumi walau aambulie pesa kwa namna yoyote.

Pia, kuna mbinu ya pili ya hadaa kutoka kwa matapeli wanaowaeleza wenye simu hoja zisizo na ukweli, lakini zinafanana kwa karibu na uhalisia wa maisha ya mpokeaji, hata akatekwa kihisia akiamini kuwapo ukweli, kumbe anaangukia mikono ya mdanganyifu.

Hapo ndipo mpokeaji anapohangaika kuhudumia matakwa ya uongo, akidhani kuna la ukweli anaouhangaikia, kumbe yuko katika mawasiliano potofu. Ni baada ya muda mfupi tu utapeli unapokamilika, simu ya mpigaji inazimwa.

Sasa kuna lingine walilolibuni inalotawala sasa, matapeli wameanzisha njia nyingine za kumpigia mtu simu na kumhusisha mtu na lililo karibu zaidi, mathalani kuwapo dharura inayomhusu mzazi au mtoto wa mwenye simu. Hapo wanasimama katika nafasi ya usamaria, wakidai wamewajibika kutumia pesa nyingi na wanahitaji kurejeshewa gharama walizoingia kutumikia dharura hiyo ya nusura, kama vile ugonjwa.

Ni aina ya taarifa inafikishwa katika hisia zenye simanzi baada ya kujitambulisha. Hicho ndicho kinachotokea kwenye shule mbalimbali sasa.

Mzazi anapigiwa simu kwamba mtoto wake ana hali mbaya ya dharura ya ugonjwa na hivyo huyo 'mwalimu' anayepiga simu, anajitambulisha kwamba wameshaingia gharama wanazohitaji kurudishiwa.

Ni hatua ambayo ama mzazi au mlezi anapowehuka na huangukia kutoa pesa kulipa pasipo kujitambua, akidhani anatatua tatizo, kumbe anawatatulia matapeli shida zao kwa mtaji wao wa hadaa.

Kuna mkasa wa ushahidi mzazi mmoja wa kike alipigiwa simu na hata katika utambulisho akahojiwa jina lake kwanza na kisha kuelezwa tatizo.

Hapo alifahamishwa kuwa wao ni walimu wako katika hospitali kubwa ya serikali jirani, wakiwa na mtoto aliyeanguka alipokuwa katika choo cha shule na ameumia anavuja damu nyingi mdomoni na puania, wakati huo anaendelea kupata matibabu.

Katika maswali yao ya awali, walimhoji kama mtoto ana kadi ya bima ya afya, kwani wao 'walimu' walipekua begi lake na hawajaona kadi. Mzazi aliwajibu 'hana.'

Hapo ndipo wakaja na hitaji watumiwe pesa za awali walizotumia 'walimu wasamaria' hao kiasi cha Sh. 30,000 na zingine zaidi kuendeleza matibabu.

Mzazi alitia shaka na kuomba akate simu muda mfupi kuweka mambo sawa, ili awatumie pesa na kisha angewapigia tena baada ya muda mfupi.

Ni hatua ambayo mzazi aliwasiliana na shule moja kwa moja, alikohakikishiwa kwamba mtoto yuko salama na anaendelea na masomo darasani.

Ufafanuzi wa ziada aliopata mzazi ni kwamba siyo tukio la hadaa ya kwanza shuleni, kuna wazazi wenzake wengi tu walishapotoshwa na matapeli kwa staili hiyo.

Baada ya mawasiliano hayo, mzazi alipiga tena simu kuwadadisi na matapeli walipobaini mzazi ni mjanja, kama ilivyo mtindo wao wa kuagana wanapogundua anayetakiwa kutapeliwa ameshtukia njama, walimtukana matusi mazito na kisha wakazima simu.

Haijaeleweka kama ndio mtindo wa makubaliano yao ya kihalifu, lakini ndio mtindo mara zote wanaaga pindi wanapogundulika kwa 'mabomu' ya matusi ya nguoni, ikifuata kuzima simu.

HABARI KITAIFA

# RC aagiza makundi ya CCM yaungane

**Na Neema Sawaka,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, amezitaka timu zote zilizokuwa zikitumiwa na watiania wa ubunge wa Msalala wilayani Kahama, kuacha tofauti zao na kuunganisha nguvu ili kupeleka maendeleo jimboni huko.

Vilevile, Zainab Telack, ameyataka makundi hayo kuungana ili kuhakikisha Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga kinashinda viti vyote vya ubunge katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba 28 mwaka huu.

Aliyasema hayo juzi muda mfupi baada ya kukamilika kwa mchakato wa kura za maoni ndani ya CCM katika Jimbo la Msalala, ambalo Idd Kassim aliongoza, akimwangusha aliyekuwa mbunge wake, Ezekiel Maige.

Telack alisema kuwa mgombea atakayeteuliwa katika vikao husika vya CCM kugombea ubunge katika jimbo hilo, aungwe mkono na watiania wengine, ili kuhakikisha ushindi mkubwa unapatikana kwa CCM uchaguzi ujao.

Mkuu huyo wa Mkoa ambaye ni mjumbe kamati ya siasa ya mkoa, aliwataka wanaCCM kuhakikisha kuwa wanamuunga mkono na kumpa kura nyingi Rais John Magufuli wakati wa uchaguzi huo.

Baada ya kutangazwa kuongoza mchakato huo wa kura za maoni, Kassim alisema kuwa kama wananchi wa Jimbo la Msalala watampa ridhaa ya kuongoza jimbo, atahakikisha linakuwa jimbo linaloongoza kwa uchumi na utajiri wilayani Kahama.

Alisema kuwa kuna baadhi ya kata ni nguzo ya kilimo katika Mkoa wa Shinyanga hususani kilimo cha mpunga na kuongeza kuwa lazima maisha ya wanaMsalala yabadilike kwa kuwatafutia masoko ya kudumu na kuwaondelea adha wakulima.

"Mimi kwa kweli nimejitoa sadaka kwenu na sina budi kuwalipa kwa kuwatumikia ipasavyo, lazima nihakikishe kuwa ninaondoa tofauti zote zilizopo baina ya viongozi walipo katika jimbo hili ili wote tufanye kazi kwa ushirikiano," alisema.

Alisema kuwa akifanikiwa kuwa mbunge, atahakikisha kuwa katika kata zote 20 za jimbo hilo, atasomesha watoto wawili kwa mwaka kwa kila kata, ili kusaidia kuinua kiwango cha elimu na kupata wasomi wengi jimboni.

# 15 washtakiwa kujipatia fedha kimtandao wa simu

**Na Hellen Mwango**

WAKAZI 15 wa Kilombero, mkoani Morogoro wamefikishwa mahakamani wakikabiliwa na mashtaka zaidi ya 20 ikiwamo kula njama na kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu kutoka kwa watu tofauti ikiwamo kutuma ujumbe mfupi wa Airtel Money na kutumia taarifa za kadi za simu isivyo halali.

Katika kesi ya kwanza, washtakiwa ni, Meniad Ndiyo (25), mkulima, dereva bodaboda Dotto Likumbai (29), Abdallah Migoi (26), mkulima na mawakala wawili Athumani Roho (28) na Onesmo Ngajela (24), ambao walisomewa mashtaka 10 mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam.

Kesi ya pili, washtakiwa Saidi Sevenjari maarufu Dangote (35), mkulima na Hasani Njalatango (34) walisomewa mashtaka sita, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Yusto Ruboroga.

Mfanyabiashara Filbert Ngatunga (26), Octavian Lekaleka (26), Francis Mhombera (24), dereva wa bodaboda Moses Mhindi (25), walisomewa mashtaka mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Richard Kabate. Michael Ngalami (21) na Omary Mbena (31) ambao ni wakala wanakabiliwa na mashtaka saba mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Agustina Mbando.

Washtakiwa wengine ni Rashid Mshamu (23) ambaye ni dereva pikipiki na wakala Emmanuel Assey (19), wanakabiliwa na mashtaka sita mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi, Rashidi Chaungu.

Akisoma mashtaka hayo, Wakili wa Serikali, Jacqueline Nyantori, alidai washtakiwa Sevenjari na Njalatango wanadaiwa kati ya Januari Mosi na Juni 15, 2020 maeneo mbalimbali wilayani Kilombero, Mkoa wa Morogoro kwa pamoja walikula njama kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Pia alidai mshtakiwa Sevenjari, kupitia ujumbe mfupi wa maandishi alituma ujumbe ukionyesha Airtel Money kwamba 'umepokea Sh. 300,000 kutoka kwa Antony Ngonyani mnamo Juni 22, mwaka huu saa mbili asubuhi salio 750,000'.

Dangote anadaiwa alijipatia Sh. 2,132,980 kutoka namba mbalimbali kwa kudanganya kwamba fedha hizo zimetumwa kimakosa arudishiwe. Nyantori alidai Mei 22, mwaka huu maeneo ya Ifakara kwa kupitia mfumo wa kompyuta mshtakiwa huyo alisambaza ujumbe kuonyesha Ngonyani alipokea Sh. 300,000 na salio lake ni 750,000 na kwamba fedha hizo zimetumwa kimakosa hivyo arudishiwe.

Pia wanadaiwa kushindwa kutoa taarifa ya mabadiliko ya laini ya simu kosa walilolitenda, Januari Mosi na Juni 15, mwaka huu maeneo mbalimbali ya Kilombero, walitumia namba za simu zilizosajiliwa kwa majina ya watu wengine bila kutoa taarifa kwa mtoa huduma.

Washtakiwa walikana mashtaka na walirudishwa rumande kwa kushindwa kutimiza masharti ya dhamana ya kuwa na wadhamini wawili wenye barua, watakaosaini kulipa Sh. milioni tano.

Hakimu Ruboroga aliahirisha kesi hiyo hadi Agosti 5, mwaka huu kwa ajili ya kutajwa.

Mbele ya Hakimu Chaungu, Wakili wa Serikali, Adolf Ulaya, alidai washtakiwa wanakabiliwa na mashtaka ya kula njama ya kutenda kosa, kusambaza ujumbe bila ridhaa ya mmiliki wa simu, kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu, kutumia namba za simu zilizosajiliwa na mtu mwingine na kutuma ujumbe kuonyesha umepokea kiasi cha fedha.

Inadaiwa walitenda kosa hilo kati ya Januari Mosi na Juni 15, 2020 Kilombero mkoani Morogoro na walikuwa na njama ya kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Ulaya alidai mshtakiwa Mshamu anadaiwa kusambaza taarifa za uongo kati ya Januari Mosi na Juni 15, 2020, Ifakara mkoani Morogoro kwa lengo la kulaghai alituma ujumbe wenye taarifa za uongo. Pia wanadaiwa kuchapisha taarifa za uongo, kosa walilolitenda Aprili 15, 2020, Ifakara Morogoro na walituma ujumbe kwa mfumo wa kompyuta wakisema "Imethibitishwa umepokea 170,000" kutoka kwa Adamson Cheyo na kusema salio lako ni 430,000".

Pia wanadaiwa kushindwa kutoa taarifa za mabadiliko ya kadi simu, kosa wanalodaiwa kutenda Januari 1, 2020 na Juni 15, 2020 Kilombero, mkoa wa Morogoro.

Pia kosa jingine la matumizi mabaya ya taarifa linamkabili mshtakiwa Assey ambapo anadaiwa kati ya Januari Mosi na Mei 30, 2020 Ifakara Morogoro akiwa Wakala wa huduma za kifedha za mitandao ya simu kwa alitumia namba mbalimbali za simu zilizosajiliwa kwa majina ya watu wengine. Wakili wa Serikali, Batilda Mushi alidai mbele ya Hakimu Shaidi kuwa washitakiwa Ndiu, Likumbai, Migoi, Tojo na Ngejela kati ya Januari 2,2020 na Juni 10,2020 wilayani Kilombero mkoani Morogoro, walikula njama kutenda kosa la kujipatia fedha kwa njia ya udanganyifu.

Washtakiwa walikana mashtaka na upande wa mashtaka ulidai upelelezi umekamilika hivyo aliomba tarehe nyingine ya kusikiliza maelezo ya awali.

Hakimu Shaidi aliwataka kuwa na wadhamini wawili wenye vitambulisho na barua watakaosaini hati ya dhamana ya Shilingi milioni mbili.




Mkuu wa Wilaya ya Ikungi, mkoani Singida, Edward Mpongolo (kushoto), akikagua msaada wa mashuka yaliyotolewa na Benki ya NMB, kwa ajili ya zahanati ya kijiji cha Iyumbu, jana. **PICHA: NATHANIEL LIMU**

# RC awapa somo waliotia nia CCM

**Na Ndalike Sonda,** KAHAMA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, amewataka vijana waliokuwa wametia nia ya kuomba kuteuliwa na Chama Cha Mapinduzi (CCM) kuwania ubunge, kuacha kusubiri muda wa uchaguzi. Badala yake amewataka kujenga mazoea ya kurejea katika majimbo yao kwa ajili ya kushiriki shughuli za maendeleo badala ya kukaa nje muda mrefu hadi mwaka wa uchaguzi.

Akizungumza mjini Kahama baada ya kumalizika kwa uchaguzi wa kura za maoni katika majimbo ya Kahama Mjini na Msalala, Telack alisema wakati wagombea wanajinadi alikuwa akisikia vijana wana elimu kubwa na kuwaomba kuitumia elimu hiyo kuleta maendeleo katika maeneo waliyozaliwa.

Telack aliwataka vijana na wagombea wengine ambao wameonekana kushindwa katika kura za maoni, kutokata tamaa badala yake iwe mwanzo mzuri wa uhusiano mazuri baina ya wananchi na CCM.

Nao baadhi ya wajumbe wa mkutano waliokuwa wanashiriki kura za maoni, walisema wilaya ya Kahama ina hazina kubwa ya vijana wasomi ambao kwa baadaye watakuwa wakombozi wa maendeleo katika jamii.

Uchaguzi wa kura za maoni kupata wagombea ubunge ndani ya CCM, ulimalizika juzi nchini kote huku safari hii vijana wengi wakijitokeza kuwania ubunge na udiwani.



Mafundi wakiendelea na kazi ya ujenzi wa daraja la juu katika makutano ya Barabara za Morogoro, Mandela na Sam Nujoma, eneo la Ubungo (Ubungo Interchange), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# JPM aibana TAKUKURU, ataka ijitathmini

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS John Magufuli, ameibana Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) juu ya ghamara za ofisi ya Chamwino mkoani Dodoma, huku akiagiza tathmini ifanyike ili kupata gharama halisi kulingana na jengo husika.

Sambamba na hilo, ameagiza kuchukuliwa hatua aliyependekeza ujenzi wa ofisi ya TAKUKURU Chato mkoani Geita wakati jengo la ofisi lipo na kusema yeye si mbinafsi, akawataka wasubiri akimaliza urais ndipo wajipendekeze.

Akizindua ofisi hiyo jana, Rais Magufuli alisema anafungua jengo hilo moyo ukiwa unamuuma, lakini anafanya hivyo kutokana na kazi kubwa inayofanywa na taasisi hiyo huku akisema kwa mwonekano wa jengo hilo lingetumia Sh. milioni 40 badala ya Sh. milioni 143.

"Huwezi kujenga nyumba kwa Sh. milioni 143. Nikacheki nyumbani nimejenga nyumba ukubwa kama huu kwa Sh. milioni 40. Tufike mahali tuwe tunazungumza ukweli. Nimehesabu mabati upande huu hayafiki 20, sasa piga upande huu na ule zidisha mara nne. Pamoja na kazi kubwa mnayofanya ambayo ni nzuri sana lazima mjitathmini," alisema.

"Mgema akisifiwa tembo hulitia maji. TAKUKURU msianze kuweka maji. TAKUKURU kimekuwa chombo ambacho hakiguswi. Naongea kama kiongozi wenu, mnatakiwa kubadilika na muanze na hili la ujenzi. Nisije nikajenga nyumba ya Sh. milioni 90 kubwa zaidi ya hii, nyie mtaondoka (wataalamu TAKUKURU) na yeye ataondoka (Mkurugenzi Mkuu)," aliongeza.

Alisema pamoja na kazi nzuri inayofanywa na TAKUKURU, takribani asilimia tano ya wafanyakazi wanafanya kazi za ovyo.

"Salamu zenu ni kung'ata lakini mama Kuluthumu aliwang'ata na inaleta picha mbaya kwamba yanapotokea mabaya ndani yenu hamshughulikiani, hadi mimi nilipotoa maelekezo kwa nini huyu? Nataka Mkurugenzi udili (ushughulike) na hii asilimia ndogo ambayo inaharibu taswira ya taasisi, licha ya mazuri yanayofanywa," alisema.

Aidha, aliitaka TAKUKURU kutumia kifungu cha 15 cha sheria yake kupeleka kesi mahakamani moja kwa moja badala ya kusubiri kibali kutoka kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP).

**ATOA ONYO**

Kadhalika, alionyesha kushangazwa na utekelezaji wa majukumu yao kwa baadhi ya maeneo ikiwamo kukamatwa kwa wabunge kwa kutoa rushwa.

"Nimesikia mtu amekamatwa hapa wa Kigoma alikuwa anatoa rushwa Dodoma sijui chooni ila za kampeni. Sijui alikuwa anagombea nini, hivi kweli Kigoma hakuna TAKUKURU? Atoke huko apite Tabora, apite Singida hadi aje Dodoma akamatwe kwa nini msimkamate huko?

Mwingine naambiwa ametoa rushwa Mtera badala ya kumkamata kwenye tukio unasubiri arudi nyumbani kwake mjini usiku ndio mumkamate. Kwa nini msimkamate hapo hapo alipokuwa anatoa kama kwenye birthday ya mtoto, huu ni mkanganyiko, kwanini hukumshikia huko na gari ulikuwa unaiona pale," alisema.

# TAKUKURU yaokoa bil. 273/- za wakulima

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) katika kipindi cha miaka mitano iliyopita imeokoa Sh. bilioni 273.38 zikiwamo fedha walizodhulumiwa wakulima.

Sambamba na hilo, taasisi hiyo katika kipindi hicho, taasisi hiyo imefungua mashauri 2,256 na 1,926 yametolewa uamuzi huku serikali ikishinda mashauri 1,013.

Akifungua ofisi za TAKUKURU jijini hapa, Rais John Magufuli alisema taasisi hiyo imerejesha mali za serikali zilizochukuliwa na watu binafsi zikiwamo nyumba na majengo 98 ikiwamo Mbeya Hotel na imewekwa kizuizini.

Naye Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, alisema TAKUKURU kwa sasa inawafanya viongozi wasimame na wajidai kwa kuwa kipo chombo kinachosimamia rushwa.

"Kuna baadhi ya maofisa wa TAKUKURU walitumika kuwadhalilisha wale wenye majimbo mlikuwa mnaenda nao sambamba kila wakiinga lakini wengine mnawaacha," alisema.

Spika wa Bunge, Job Ndugai, alisema wako Watanzania waongo ambao wanataka TAKUKURU ifanye kazi kwa maslahi yao.

"Kama mtu hampendi kiongozi wake anataka atolewe ili apande yeye cheo. Watu wa namna hiyo waache maana taasisi hii ina heshima kubwa. Wanaotoa taarifa feki na wenyewe wang'atwe na TAKUKURU mkigundua ilikuwa na dhamira mbaya," alisema.

Aidha, alisema TAKUKURU imefanya kazi kubwa katika kura za maoni za Chama Cha Mapinduzi (CCM) na kuwataka katika uchaguzi mkuu wafanye zaidi na wasimamie na kwenye vyama vingine vya siasa.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, alisema kazi iliyofanywa na taasisi hiyo kwa miaka mitano imeanza kuleta matumaini makubwa.

"Kazi kubwa imefanywa ya kupambana na rushwa nchini kwa kipindi cha miaka mitano, na tumeanza kuona nidhamu kwenye maeneo ya utoaji huduma, ambayo walikuwa wakiomba rushwa na kufanya wananchi kushindwa kuwasilisha kero zao kutokana na kudaiwa rushwa," alisema.

Alisema Watanzania wana wajibu wa kutoa taarifa za vitendo vya rushwa ili hatua zichukuliwe na vitendo hivyo vikome.

Naye Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, alisema kuna mahitaji ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa uzio, uwekaji wa mfumo wa TEHAMA na samani kwenye ofisi hizo zilizojengwa.

Awali, Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi hiyo, Brigedia Jenerali John Mbungo, alisema katika mwaka 2017/18 Rais alitoa Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi wa majengo saba ya taasisi hiyo ngazi ya wilaya.

"Yamejengwa kwa aina moja ya mchoro na ujenzi wake umetumia mfumo wa 'force account' na yamejengwa kwa muda ndani ya miezi saba hadi 12 chini ya usimamizi wa wataalamu wa TAKUKURU," alisema.

Aidha, alisema watumishi 1,755 walipandishwa vyeo katika mwaka wa fedha 2019/20 ambapo mara ya mwisho kupandisha ilikuwa mwaka 2013/14.

"Katika mwaka wa fedha 2019/20 tunatarajia kujenga ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Morogoro, pia ujenzi wa Makao Makuu ya TAKUKURU Dodoma. Tayari tumepatiwa Sh. bilioni moja kwa ajili ya ujenzi na eneo," alisema.

# H/shauri zatakiwa kuhamasisha kilimo

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKOA wa Morogoro umeziagiza Halmashauri zake kuhamasisha makundi ya vijana, wanawake na walemavu wanaopatiwa mikopo itokanayo na makusanyo ya ndani kuwekeza kwenye kilimo cha mazao ili kukuza mapato la serikali.

Wito huo ulitolewa jana na Katibu Tawala wa mkoa huo, Mhandisi Emmanuel Kalobelo, kwa kuzitaka halmashauri zote za mkoa huo kutenga fedha asilimia 10 ya mapato yote ya ndani kuhamasisha kilimo kupitia makundi hayo.

"Ili vikundi hivi viweze kuwa na tija, vinatakiwa kuwekeza kwenye kilimo cha mazao mbalimbali katika maeneo yao, hivyo viongozi wa halmashauri kupitia idara husika hakikisheni vikundi hivi vinawekeza kwenye kilimo," alisema Kalobelo.

Kalobelo alisema kilimo cha mboga na matunda kina tija kwa wajasiriamali nchini kupitia vikundi vyao, hivyo endapo watawekeza kwenye kilimo cha mazao hayo yatawasaidia kuimalisha uchumi wao wa kila siku.

Alisema halmashauri kama za Mvomero na Gairo ni maarufu kwa kilimo cha matunda na mboga, hivyo endapo wakulima kupitia makundi yao ya ujasiriamali yatawezeshwa watazalisha mazao mengi hali itakayoongeza pato la taifa.

Alisema kuwa halmashauri nyingi za mkoa huo zinategemea mapato ya ndani kutokana na sekta ya kilimo cha mazao mbalimbali hivyo ipo haja ya kuboresha kilimo kupitia vikundi vyote cha ujasiriamali ili kukuja pato la taifa.

Alisema ili halmashauri hizo ziweze kuwa na mapato mazuri, suala la uhamasishaji wa kilimo chenye tija ni la kuzingatia sana kwani ndiyo uti wa mgogo wa taifa, hivyo alizitaka halmashauri kuhakikisha vikundi vinawekeza kwenye kilimo.

Naye Mwenyekiti wa kijiji cha Mkuyuni Kata ya Mlali, Hamisi Nyagalile, alisema wananchi wanashawishika kulima mazao hayo, lakini tatizo kubwa ni kutokuwa na vituo maalumu vya kuuzia badhaa zao baada ya mavuno kutoka shambani.

Nyangalile alisema kijiji chake kina kituo cha kukusanyia mazao hayo, lakini hakifanyi kazi licha ya kwamba kimejengwa kwa gharama kubwa, na kuiomba serikali iwasaidie suala hilo ili kituo kianze kufanya kazi iliyokusudiwa.

## HABARI KITAIFA



Mwezeshaji Mariam Tambwe, akiendesha semina kwa wafanyabiashara wanawake wa nje ya mipaka ya Tanzania iliyoandaliwa na Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP), jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Likizo ya corona ilivyoibua wanafunzi wenye ujauzito

**Na Zuwena Shame,**
IRAMBA

WIMBI la mimba za utotoni limekuwa tatizo kwa baadhi ya wanafunzi wa kike kuwa moja ya chanzo cha kukatisha ndoto zao kielimu na kimaisha.

Wakati wa likizo ndefu ya ugonjwa wa corona katika Halmashauri ya Wilaya ya Iramba, mkoani Singida, tatizo hilo lilijitokeza hasa kwa wanafunzi wa shule za sekondari.

Wilaya ya Iramba ina shule za sekondari za serikali zipatazo 22 na binafsi mbili na tatizo la ujauzito mara nyingi hutokea kwa shule za sekondari.

Baada ya serikali kufungua shule zote nchini mwishoni mwa mwezi ulipita, changamoto ya ujauzito kwa wanafunzi wa kike ilionekana wilayani humo.

Uchunguzi wa Nipashe uliofanywa kwa wiki mbili katika shule mbalimbali za sekondari wilayani humo, umegundua kuwa zaidi ya wanafunzi saba walikutwa na ujauzito baada ya likizo ya corona na wanne kati yao ni kutoka shule moja.

Akizungumza na Nipashe, Mkurugenzi Mtendaji wa manispaa hiyo, Linno Mwageni, alikiri kuwa tatizo la mimba kwa wanafunzi hasa shule sekondari lipo na hivyo kumekuwa na mikakati endelevu mojawapo ikiwa ni kuwapima mimba wasichana baada ya kufungua shule.

Mwageni alisema lengo la zoezi hilo ni kutaka kujua kiasi cha tatizo na kuchukua hatua stahiki jinsi ya kuwasaidia wasichana wilayani humo kwa kuwapa elimu ya athari za mimba wakiwa wanafunzi.

Kadhalika, Mwageni alisema kuwasuala hilo litasaidia kuchukua hatua za kisheria kwa watakaobainika kuwa wahusika wa mimba hizo kutokana na kuharibu ndoto za baadaye na malengo ya wanafunzi wa kike.

Mwageni alisema kuwa wanashirikiana na walimu wakuu wa shule hizo kwa kuwapima wanafunzi mimba kwa siri na baadaye kushirikiana na jeshi la polisi kwa ajili ya kuwachukulia hatua za kisheria wahusika wa mimba hizo.

Alisema kuwa baada ya likizo ya ugonjwa wa corona, zoezi la kuwapima mimba wanafunzi wa kike ni la lazima kwa kuwa likizo ilikuwa ndefu na ili kubaini changamoto hiyo ni vyema kuwaangalia na kuchukua hatua za tahadhari kwa likizo zingine zijazo.

"Likizo ya corona imekuwa ndefu na tangu tumefungua shule tumeshaaza kuwapima wafunzi wa kike mimba ili kujua hatua stakihi za kuchukua. Likizo ya corona imeleta shida kwa upande wa elimu hasa wasichana alisema Mwageni.

Aliongeza kuwa serikali imekuwa ikikosa ushirikiano kutoka kwa wazazi wa wanafunzi wanaokutwa na mimba na hivyo kukosa nguvu ya kuchukua hatua za kisheria na namna ya kutatua tatizo hilo.

Alisema kuwa baadhi wazazi wakishajua watoto wao wana ujauzito huwatorosha na wengine kufanya kama biashara na wahusika wa mimba hizo kwa kuwapa fedha au ahadi za ndoa.

"Zoezi hili tunafanya kwa siri kubwa kwani mara nyingi baadhi ya wazazi wanapogundua kuwa binti zao wana ujauzito huwatorosha na kuelewana na wahusika wa mimba hiyo, hivyo upande wetu tunakosa nguvu za kuendelea kufatilia kesi hiyo," alisema.

Alisema kuwa zoezi hilo hufanyika kwa ushirikiano wa viongozi wa wilaya, maofisa elimu, walimu wakuu, jeshi la polisi na zahanati zilizopo karibu na shule.

Alipoulizwa kuhusu idadi ya wanafunzi waliokutwa na ujauzito tangu kuanza kwa zoezi hilo, Mwageni alisema kuwa takwimu sahihi zitatolewa mwishoni mwa mwezi huu.

Ofisa elimu (Sekondari) wa wilaya hiyo, Mwanjala Godfrey, alisema tatizo la mimba kwa wanafunzi wa kike limekuwa haliishi kutokana na baadhi ya tamaduni na wazazi kuwa na malezi mabaya na kuwaficha watoto wao.

"Tamaduni na malezi ya wazazi zinachangia suala hili kwa namna moja au nyingine, wanafunzi wanapokuwa shuleni walimu wanatimiza wajibu wao wa kuwaangalia na kuwabana wasijiingize kwenye masuala ya ngono ila wanapokuwa likizo ndio wanakopata ujauzito," alisema Godfrey.

Vilevile, alisema likizo ya corona imewafanya waweke mkazo thabiti kwenye zoezi la upimaji mimba kwa kuwa wanafunzi walikaa nyumbani kwa muda mrefu ikilinganishwa na likizo zingine.

Alisema kuwa wanafunzi wengi wanaokutwa na mimba ni kidato cha pili na tatu.

# JPM awashukuru wazee kumchangia 100,000/-

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS John Magufuli amewashukuru wazee wa Wilaya ya Nachingwea mkoani Lindi kwa mchango wao wa Sh. 100,000 walioutoa ili umsaidie katika uchaguzi.

Julai 13, mwaka huu, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa katika uwanja wa ndege wa Nachingwea, alipokea mchango huo kwa niaba ya Rais Magufuli kutoka kwa wazee hao.

Akitoa salamu hizo kwa niaba ya Rais Magufuli jana katika uwanja wa ndege wa Nachingwea, Majaliwa alisema Rais amefarijika sana kwa mchango huo.

"Rais amesema aliniona wakati napokea salamu kutoka kwa wazee hapa uwanja wa ndege Nachingwea, mkanikabidhi mchango kwa ajili yake. Anawashukuru sana na salamu zenu amezipokea kwa mikono miwili," alisema.

Waziri Mkuu alisema Rais Magufuli anawashukuru kwa kupata wazo hilo na akawataka waendelee na majukumu yao na kuahidi kuzunguka maeneo yote nchini ili kuwapa mrejesho wa utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2015 - 2020.

Akizungumzia mchakato wa kura za maoni ndani ya CCM, Majaliwa aliwapongeza wana CCM waliojitokeza kwa wingi kuomba ridhaa ya kuteuliwa kuipeperusha bendera ya CCM katika mchaguzi mkuu ujao na kuwataka wataka waendelee kuwa wamoja.

"Endeleeni kuwa wamoja hata baada ya mchakato wa kumpata mgombea mmoja wa kupeperusha bendera ya CCM kukamili na ninawasihi wote muunge mkono mgombea huyo ili kujenga mshikamano na kuki chama ushindi," alisema.

Majaliwa alisema hayo baa ya kubaini kuwa miongoni m wananchi waliojitokeza kwe Uwanja wa Ndege wa Nachi wea kumuaga wakati akitoka angwa kurejea Dodoma ni wa CCM waliojitokeza kuom ridhaa ya chama kwa nafasi ubunge na ambao wamemal mchakato wa awali wa kupigi kura.

## TAKUKURU yawanoa watumishi Manispaa

**Na Friday Simbaya, IRINGA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Iringa kwa kushirikiana na Shirika la Konrad Adeneur Stiftung (KAS) la Ujerumani, imeendesha mafunzo kwa baadhi ya watumishi wa serikali za mitaa wa Manispaa ya Iringa.

Katika mpango huo, zaidi watumishi wa serikali za mitaa 40 wamepatiwa mafunzo katika mada mbalimbali zikiwamo rushwa na maadili, makosa ya rushwa kwa mujibu wa Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (PCCA) Na. 11 ya mwaka 2007, vitendo vya rushwa katika uchaguzi, juhudi za serikali katika kudhibiti rushwa nchini, ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma (PETS) na wajibu wa ulinzi wa mwananchi katika kupambana na rushwa.

Akizungumza na jana wakati wa mafunzo hayo, Mkuu wa TAKUKURU Mkoa wa Iringa, Mweli Kilimali, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwajengea uelewa watumishi wa mamlaka za serikali za mitaa, hususani Manispaa ya Iringa kuhusu mapambano dhidi ya rushwa.

Kilimali alisema rushwa ni tatizo la kidunia lenye madhara kwa taifa na kuongeza kuwa inaua demokrasia na kuangamiza utawala wa sheria na kusababisha ukiukwaji wa haki za binadamu.

Pia alisema rushwa ni chanzo kimojawapo cha matumizi mabaya ya rasilimali za umma, utoaji wa huduma duni kwa umma na kuchangia kuongezeko kwa vitendo vya uhalifu na vitendo vingine vinavyoathiri usalama wa nchi.

Alisema kuwa ukiukwaji wa maadili kwa watumishi pamoja na mmomonyoko wa maadili wa jamii ndicho chanzo kikuu cha kuongezeka kwa vitendo vya rushwa na kusababisha utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya kiwango.

Naye Mkurugenzi wa Manispaa ya Iringa, Hamid Njovu, alizipongeza TAKUKURU na KAS kwa kuaandaa mafunzo hayo muhimu ya kujenga uwelewa wa watumishi wa mamlaka za serikali za mitaa kuhusu elimu ya mapambano dhidi ya rushwa.

Alisema vitendo vya rushwa katika manispaa vimepungua kutokana na jamii kuwa na elimu juu ya rushwa.

Njovu alisema kumekuwapo na malalamiko ya vitendo vya rushwa lakini kutokana na kuwapo kwa kamati za kudhibiti uadilifu na kupitia mafunzo yanayotolewa na taasisi ya kuzuia na kupambana na rushwa kumepunguza vitendo hivyo.

Mwakilishi wa Mkurugenzi wa KAS, Damas Nderumaki, ambaye pia ni Meneja Mradi wa Tuungane Kutetea Haki, alisema TAKUKURU iliingia makubaliano na (KAS) kushirikiana katika kuelimisha na kuhamasisha ushiriki wa wananchi na serikali za mitaa katika kupambana dhidi ya rushwa.

Alisema mafunzo kwa watumishi wa serikali yataboresha utendaji kazi kwa na hatimaye kupunguza vitendo vya rushwa katika jamii, kuboresha huduma kwa jamii, kupunguza umasikini na kuwepo kwa maendeleo endelevu.

# Wenye ulemavu watakiwa kutumia fursa

**Na Frank Kaundula,**

MOROGORO

WATU wenye ulemavu wametakiwa kutumia vizuri fursa zilizipo ambazo zimekuwa zikitolewa na serikali katika nyanja mbalimbali kama vile kuanzisha vikundi vya ujasiriamali ili kujikwamua kiuchumi.

Mwenyekiti wa Chama cha Wanawake na Watoto wenye Ulemavu Tanzania, Nuru Awadhi, alisema hayo jana wakati wa semina iliyoandaliwa na Shirikisho la Vyama vya Watu wenye Ulemavu Tanzania (SHIVYAWATA) mjini hapa.

"Serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa makundi mbalimbali likiwamo kundi la wenye ulemavu, hivyo napenda kutoa rai yangu kwenu kwamba mnatakiwa kuzitumia vizuri fursa hizo ili kujipatia kipato cha kutosha," alisema.

Awadhi alisema kitendo cha wenye walemavu kuwa na makundi mbalimbali ya ujasiriamali ni jambo zuri kwa kuwa inasaidia kuwa na vigezo vya kupata mikopo kutoka kwenye taasisi za kifedha na kuwawezesha kuwa na mitaji.

SHIVYAWATA, alisema imeamua kutoa semina ili kuwaelimisha wenye ulemavu nchini hususani mkoa wa Morogoro kutambua umhimu wa kuzitumia vizuri fursa zinazotolewa na serikali.

Alisema endapo watu wenye ulemavu nchini watazitumia fursa vizuri zinazotolewa na serikali ya Rais Magufuli watanufaika kiuchumi kupitia miradi mbalimbali ya ujasiriamali kitendo kitakachowafanya wauondoe utegemezi.

Mwenyekiti wa Chama cha Watu Wenye Ualbino Tanzania (TAS) Mkoa wa Morogoro, Hassan Mikazi, aliishukuru serikali kwa kuwatazama walemavu hususani watu wenye ualbino na kusema watahakikisha wanazifanyia kazi fursa zote.

Alisema lengo la chama chake ni kutaka kuona wanajikwamua kiuchumi kupitia fursa zote zilizopo na zitakazoendelea kujitokeza hivyo watahakikisha wanashiriki kikamilifu ili kuweza kupunguza changamoto mbalimbali zinazowakabili wao.

Naye Ofisa Maendeleo ya Jamii Mkoa wa Morogoro, Saada Mustapha, alisema anatekeleza sera elekezi ambazo zimekua zikiwasaidia walemavu katika vikundi vyao ambapo amewataka kujitokeza kuwania nafasi mbalimbali za uongozi.

# Watanzania waondolewa hofu kuadimika mafuta

**Na Joseph Mwendapole**

WAKALA wa Uagizaji Mafuta Pamoja (PBPA), umesema kuna akiba ya kutosha ya mafuta nchini na kuwataka Watanzania wasitarajie kuona upungufu kutokana na mifumo thabiti waliyoweka.

Kaimu Mkurugenzi Mkuu wa PBPA, Erasto Mulokozi, alisema hayo jana alipokuwa akizungumzia mafanikio na changamoto tangu kuanzishwa kwa mfumo huo mpya wa kuagiza mafuta mwaka 2015. Alisema wamekuwa wakifuatilia kwa karibu matumizi ya mafuta kila siku na akiba iliyopo, hivyo suala la uhaba wa nishati hiyo haliwezi kutokea kwa mfumo waliojiwekea wa ufuatiliaji.

Mulokozi alisema hata maneno yaliyotokea hivi karibuni kwamba baadhi ya mikoa ilikuwa na upungufu wa mafuta, ulikuwa uzushi na hila za baadhi ya waagizaji na ndiyo sababu Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) iliingilia kati na kulimaliza. Alisema kanuni inataka kila kampuni ya mafuta iwe na akiba ya kujiendesha kwa siku 15 mbele lakini PBPA imekwenda mbali zaidi kwa kuweka hadi siku 40 ili kuhakikisha mafuta ya akiba yanakuwapo hata meli yenye shehene mpya ikichelewa.

"Meli kutoka mashariki ya kati ambako asilimia 70 ya mafuta yetu tunayatoa huko inatumia wastani wa siku 10 au 14 kutegemea na hali ya hewa. Sasa huwezi kujua kitakachotokea ndiyo sababu tunajitahidi kuweka akiba ya muda mrefu," alisema Mulokozi

"Mafanikio mengine ni kwamba hivi sasa tunajua mwezi Agosti na Septemba ni kiasi gani cha mafuta kinatarajiwa kuingia nchini lakini zamani haikuwa hivyo kwani ulikuwa huwezi kujua kiasi cha mafuta kinachotarajiwa kuingia nchini mpaka siku yatakapofika," alisema Mulokozi alisema mafanikio mengine ni kuanzishwa kwa sehemu zingine za kupokelea mafuta kutoka moja iliyokuwepo kabla ya mwaka 2015 hadi kufikia tatu ambazo ni Dar es Salaam, Tanga na Mtwara.

Alisema zamani ilitegemewa Kurasini Dar es salaam tu kama sehemu ya kupokelea shehena ya mafuta jambo ambalo ni hatari kama ikitokea dharura kwani shehena haitaweza kupakuliwa na kusababisha taharuki.

Mulokozi alisema nchi jirani za Zambia, Malawi, DRC, Rwanda na Burundi zimefurahishwa na mfumo huo na zinapitisha mafuta yake Tanzania.

"Zamani asilimia 20 mpaka 30 ya mafuta tuliyokuwa tukiagiza yalikuwa ya nje ya nchi (on transit cargo) lakini kwa sasa yanayopita nchini yameongezeka hadi kufikia asilimia 49 wakati asilimia 55 ni ya matumizi ya hapa nchini," alisema Mulokozi Alisema shughuli nyingi za kiuchumi zinategemea zaidi mafuta hivyo mamlaka hiyo muda wote inatakiwa kuwa macho kufuatilia kujua kiasi cha mafuta kinachotumika, kilichopo na kinachotarajiwa kuwasili nchini.




Meneja Mawasiliano wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dar es Salaam (DAWASA), Everlasting Lyaro (kulia) na Meneja wa Majitaka, Joyce Mwanjee (kushoto), wakitoa ufafanuzi kuhusu usajili wa magari ya majitaka unaoendelea kwa mmoja wa dereva wa magari hayo aliyefika katika mabwawa ya Vingunguti, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kusajiliwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# NGO zatakiwa kuendesha miradi yenye tija

**Na Mwandishi Wetu,**
MUFINDI

MWENYEKITI wa Bodi ya Uratibu wa Mashirika yasiyo ya kiserikali Dk. Richard Sambaiga, ameyataka mashirika yasiyo ya kiserikali kuhakikisha miradi wanayoifanya inawaongezea tija wananchi.

Dk. Sambaiga aliyasema hayo wilayani Mufindi, Iringa wakati akikagua utekelezaji wa miradi ya kilimo, ufugaji na mpango wa matumizi bora ya ardhi inayofanywa na Shirika la PELUM Tanzania katika vijiji vya Kipanga na Lilongole.

"Kuna umuhimu kwa hawa wananchi wanaofanya kilimo au ufugaji wafanye kwa namna ambayo itawaongezea tija, kuliko kuona wanatumia nguvu nyingi, lakini tija kidogo," alisema Dk. Sambaiga.

Alisisitiza mwenendo wa mashirika kuripoti kazi walizofanya na kufanikiwa, ziendane na kuongeza ufanisi katika utendaji kazi ili miradi hiyo iwe mfano na kuhamasisha wengine kujiunga.

"Tuongeze vipengele vya kuwezesha utaalamu wa kilimo na ufugaji uwe wa kisasa ili kuongeza tija na miradi hiyo iwe ni mfano," alisema.Naye Msajili wa Mashirika yasiyo ya kiserikali, Vickness Mayao, aliyataka mashirika hayo kutoa taarifa mara kwa mara kwa wananchi kuhusu kazi zao na kuboresha majukumu wanayoyafanya.

"Bado tunahimiza mashirika kutekeleza majukumu yao kwenye eneo walilosajili, wanaweza kuongeza thamani ya miradi yao bila kuathiri lengo lao," alisema Mayao.

Akiwasilisha taarifa ya mradi huo, Mratibu wa shirika hilo, Donati Senzia, alisema, shirika kwa kushirikiana na Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, inatarajia kupima mashamba zaidi ya 500 ili wananchi hao wapewe hati na ardhi ili kuwanufaisha kiuchumi.

"Tuliona kwenye mradi huu tusiishie tu kupima bali tuangalie ardhi itawanufaishaje wananchi kiuchumi hasa kwa kinamama," alisema Senzia.

Naye Ofisa Ardhi wa Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi, Simon Mbag, amesema wanashirikiana na mashirika mbalimbali kuhakikisha wananchi wananufaika na ardhi kwa kuwapimia na kubainisha matumizi ya ardhi.

Baadhi ya wanufaika wa vijiji hivyo wameelezea kufurahishwa na PELUM hususani kupata elimu ya kumiliki na kuitumia ardhi kwa manufaa na kupunguza migogoro ya ardhi kwa kiwango kikubwa.

Hata hivyo, wananchi wengi waliomba serikali kwa kushirikiana na NGO kuwasaidia kutatua kero ya barabara na maji ili kuwawezesha kujikita katika kilimo.

"Kipaumbele kwetu ni barabara kwa kuwa hata haya mazao hatuwezi kuyafikisha kwenye masoko, barabara yetu inapitika katika msimu mmoja tu, wakati wa mvua hatuwezi kufika mjini," alisema mmoja wa wanakijiji.

Ziara ya ukaguzi wa kazi za mashirika yasiyo ya kiserikali inakusudia kujiridhisha dhidi ya taarifa zinazowasilishwa katika Ofisi ya Msajili na thamani halisi ya fedha zilizotumika katika maeneo ya miradi.



Ukurasa 12

**Wadau wanaonusuru wachimba madini madhara zebaki**



Ukurasa 13

Hii ndio maana ya shinikizo la damu, yake yaliyojificha




Ukurasa 14

**Namna ulivyo uzazi, idadi ya watu inavyoshuka duniani**

AFYA

# Mradi wafuta Km. 5 safari za maji, maisha mapya hawakutani na fisi

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

UNAPONZUGUMZA leo na wanakijiji wa Uzongole ndani ya Manispaa ya Shinyanga, wana mengi kuhusiana na maji shida ya maji.

Mara baada ya kuzinduliwa mradi wa maji kijijini humo, kutokana na huduma ya maji kupatikana umbali mrefu, waathirika wakuu kinamama waliofunga safari za alfajiri, kuanza mchakato wa kilomita kadhaa, hadi saa tatu, ilikuwa hoihoi.

Hapo kuna simulizi za ziada za ugomvi wa wanandoa, kukutana na fisi wa Shinyanga, hata maofisa wanyamapori wanaopata tabu kuwanasa, pindi wanaporipotiwa malalamiko, nao huishia katika matatizo.

Kuzinduliwa mradi huo wa maji kijijini Uzongole, leo inabaki kuwa kinachoitwa na wasomi wa lugha "ya wakati uliopita." Sera ya Maji kitaifa inawataka watu kuwa nayo katika umbali usiozidi mita 400.

Mtazamo mkuu wa kinamama katika hafla hiyo ya uzinduzi ni hoihoi, chereko na nderemo iliyowatawala uzinduzi miezi michache, maana hao ndio waathirika wakuu wakiwajibika wanahakikisha maji yanakuwapo ndani ya makazi muda wote.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Uzongole, Peter Ngwatu, anasema wakazi wa kijiji hicho wapatao 3,378, kwa miaka mingi wametaabika kufuata maji umbali mrefu.

"Tunashukuru sana kuzinduliwa mradi huu wa maji safi na salama hapa kijijini kwetu na umetupatia kiburi hata kuitisha mikutano ya hadhara.




Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mbokeo (kulia), akimtwisha ndoo ya maji kichwani Kibibi Elias, baada ya kuzindua mradi wa maji safi na salama kutoka Ziwa Victoria, katika kijiji cha Uzongole, Manispaa ya Shinyanga. **PICHA: MARCO MADUHU**

> **Walifuata maji safi na salama kwenye kijiji jirani cha Ikulilo na ndipo palipopatikana mikasa ya kukutana na fisi.**

"Sababu awali tulishindwa kufanya hivyo, kwa kuogopa kulizwa maswali ya lini tutawaondolea wananchi changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama," anasema Ngwatu.

Kaimu Meneja Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (Ruwasa) Wilaya ya Shinyanga, Emmanuel Nkopi, anasema mradi wa maji safi na salama kijiji walianza kuutekeleza Februari 5, mwaka huu kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira Mjini Shinyanga (Shuwasa) na ulikamilika Mei 6.

Agnes Dotto, ni mwanamama anayeishi kijijini Uzongole, anasema kabla ya kuzinduliwa mradi walikuwa wakifuata maji katika kijiji jirani cha Ikulilo, umbali wa kilomita tano.

Mama huyo anasema, walilazimika kufuata maji safi na salama kwenye kijiji jirani cha Ikulilo na ndipo palipopatikana mikasa ya kukutana na fisi.

"Tunafurahi sana kuzinduliwa mradi wa maji safi na salama hapa kijijini kwetu, tena maji kutoka Ziwa Victoria, ambayo yatatuondolea matatizo ya kufuata maji umbali mrefu," anasema Dotto.

Regina Msabila, anaelezea shida na athari za muda zilizowafikia, walichoka zaidi hata kuwarudisha nyuma kimaendeleo.

Anarejea kipindi cha kiangazi, jumuiya ilipata tabu kubwa ya vyanzo vya maji hata wakataabika, hata katika sababu zinazoambatana nazo.

"Tunashukuru sana kuzinduliwa mradi huu wa maji safi na salama hapa kijijini kwetu na umetupatia kiburi hata kuitisha mikutano ya hadhara.

"Sababu awali tulishindwa kufanya hivyo, kwa kuogopa kulizwa maswali ya lini tutawaondolea wananchi changamoto ya ukosefu wa maji safi na salama," anasema Ngwatu.

Mradi huo umegharimu Sh. milioni 88.8 na Ruwasa imechangia Sh. milioni 50.4; Shuwasa Sh.milioni 31.6; na nguvu za wananchi Sh. milioni 6.7.

"Lengo kuu la kutekeleza miradi hiyo ya maji vijijini ni kutekeleza Sera ya Maji ya Mwaka 2002, kwamba wananchi wa kijijini wanapaswa kupatiwa maji safi na salama kwa asilimia 85," anasema Nkopi.

Mkurugenzi wa Shuwasa, Flaviana Kifizi, anasema: "Kutokana na mradi huu wa maji safi na salama kuwa hapa kijijini kwenu Uzongole, naombeni sasa mlipie pesa ili tuje tuwavutie maji hadi majumbani kwenu, ili mpate kufaidika nayo vizuri muwe na maji ndani na siyo kubeba tena kichwani ili tumtue ndoo kichwani mwanamke."

Mkuu wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, anawataka wananchi wa kijiji hicho cha Uzogole kuitunza miundombinu ya mradi .

AFYA

# Wadau wanaonusuru wachimba madini kutoka madhara zebaki

• Shida jibu la 'mbadala uko wapi?' • Angalizo; athari kiafya zinatisha



Ndivyo ilivyo, kazi ya uchenjuaji dhahabu kwa kutumia zebaki. **PICHA: MTANDAO**

**Na Marco Maduhu,** ALIYEKUWA

GEITA

UNAPOTAJA zebaki, hiyo ni kemikali maarufu inayotumiwa na wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu kwa ajili ya kukamata dhahabu wakati wa kuichenjua kwenye mchanga wenye madini hayo.

Ufundi wake ni kwamba kemikali inawekwa kwenye karai lenye mchanga wa madini ya dhahabu na maji kwa ajili ya kukorogwa kwa mikono, ili iweze kukamata dhahabu.

Kinachoelezwa katika misingi ya afya kuwa hatari, ni pale itakapopenya mwilini mwa mwanadamu, huku kukiwapo maelezo wachimbaji madini wadogo wengi hawazingatii usalama huo, pindi wanapowajibika kuchenjua zebaki.

Miongoni mwa zana kinga anazozitaja ni vifaa kinga kama vile kofia ngumu, nguo maalumu, viatu ya usalama kinga za mkono - glovu.

Inaelezwa kwamba, hali ya kutovaa vifaa kinga hivyo hatari iliyopo ni kwa wahusika wanapopatwa na michubuko, wanaingia katika hatari ya uwezekano mkubwa zebaki kuingia mwilini na kuwaletea madhara kiafya.

Ni aina ya tatizo na madhara yaliyotokea katika mji mmoja nchini Japan mwaka 1956, wafanyakazi wa kiwanda cha maji taka waliathirika na kemikali na zebaki.

Historia inaonyesha waliugua ugonjwa huo uitwao Minamata, wafanyakazi walioathirika na ugonjwa huo,walipatwa na homa kali, kifafa na kuharibika figo, hata kupoteza kumbukumbu haraka, hali iliyosababisha kuwapo vifo vya haraka.

> "Lengo la kampuni ni kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu waondokane na uchimbaji ambao siyo salama kwa afya zao, kutokana na kutumia vifaa duni na kemikali ya zebaki kukamatia dhahabu ambayo siyo salama kiafya.

### ZIARA GEITA

Mwaka huu Nipashe ilizuru migodi ya madini dhahabu, iliyopo mkoa wa Geita na kupata ushuhuda wa ukiukaji wa kanuni hizo za afya, ukamataji zebaki pasipo kujali kanuni na miongozo ya kiafya.

Hadi sasa sehemu kubwa ya wachimba migodi midogo wanatumia kemikali zebaki na kati yao kuna idadi kubwa ya wasiotumia vifaa kinga vinavyosaidia kuwaepusha na madhara ya zebaki mwilini.

Katika ziara yake wilayani Mbogwe, Geita, Nipashe ilishuhudia kampeni ya kampuni moja ya wazawa imeanza mikakati kusaidia wachimbaji wadogo wao ndokane na matumizi hayo ya zebaki.

Juma Mgoja, Meneja wa kampuni hiyo anasema baada ya kuona ukiukwaji huo wa kanuni za kiafya katika kampuni hiyo, wachimbaji hao wadogo wamebuni mbadala unaoweza kutumika kukamata dhahabu pasipo kutumia kemikali.

Anasema walianza na utafiti kwa mradi unaowakusudia wachimbaji wadogo kuacha kutumia zebaki na watakuwa wakiwakopesha vifaa kupitia vikundi na akabainisha mradi huo utawafikia wachimbaji wote wa mkoa Geita.

"Matarajio ya kampuni yetu ni kuona wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu mkoani Geita, waondokana na matumizi ya kemikali ya zebaki kukamata dhahabu.

"Watakuwa wakitumia mfumo wa mtambo wenye 'process' nzima wa ukamataji dhahabu bila ya kutumia kemikali yoyote.

"Vifaa hivi vya kukamata madini ya dhahabu bila ya kutumia kemikali yoyote, tutakuwa tunavitoa kwenye vikundi kwa kuingia nao makubaliano ya asilimia fulani, wakiuza madini na sisi kuna asilimia yetu hadi pale tukaporudisha gharama zetu za vifaa hivyo," anaongeza.

Aidha, Mgoja anafafanua kuwa wanatarajia kuwapatia vifaa kinga vya kitaalamu, kwa ajili ya matumizi ya kuchimba madini, zikiwamo glovu, mavazi, viatu na winchi la kutoa nje mawe yenye madini ya dhahabu, ili kuongeza kasi ya uzalishaji.

### OFISA MADINI NA WACHIMBAJI

Ofisa Madini Mkoa wa Geita, Daniel Mapunda, anasema serikali na mashirika mbalimbali bado wanaendelea kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo kuhusu madhara ya kutumia zebaki.

Ni elimu inayotolewa kupitia mikutano na warsha mbalimbali, pia ushauri kwa watumiaji vifaa kinga wakati wa kuchenjua madini, lengo ni waishie katika usalama.

Anasema, hadi sasa serikali imeshaingia kwenye mkataba wa kimataifa wa kuyaondoa matumizi ya zebaki kwa wachimbaji wadogo na wahamie mbadala uliopo katika uchenjuaji dhahabu.

Mapunda anaeleza njia hizo zina gharama kubwa na wachimbaji wadogo hawawezi kuzimudu ambacho watakifanya, ni kuendelea kuwabadilisha taratibu.

"Serikali inafahamu kabisa madhara ya matumizi ya zebaki wakati wa kukamata dhahabu, lakini tukisema leo tuzuie kabisa matumizi ya zebaki nadhani tutaathiri sekta ya uchimbaji kwa sababu zebaki ina gharama ndogo na rahisi kupatikana.

"Ndio maana tunaendelea kushirikiana na mashirika na kampuni mbalimbali, ili kuwasaidia wachimbaji hawa wadogo wa madini ya dhahabu kuondokana na matumizi ya zebaki, pamoja na kuvaa vifaa kinga wakati wa uchimbaji madini ili kulinda usalama wao," anasema Mapunda.

Saidi Kweji, mmiliki wa eneo la uchimbaji dhahabu, wilayani Mbogwe, anakiri kutambua madhara ya kutumia zebaki katika kukamatia madini dhahabu, lakini wanashindwa kuepuka, kwa sababu ya kukosa mbadala.

"Tunaipongeza kampuni hii inayotaka kutusaidia sisi wachimbaji wadogo kutupatia vifaa vya kisasa vya uchimbaji madini," anasema Kweji, akiongeza kwa lugha ya tahadhari:

"Pamoja na kuondokana na matumizi ya zebaki ambayo ni hatari kwetu, lakini kutokana na hakuna njia zingine mabadala kuwa za gharama, ikatubidi tuendelee kuitumia tu licha ya kujua ina madhara kiafya."

Japhet Ntelezu, ni mchimbaji dhahabu wa wilayani Mbogwe, analia ukosa mbadala wa nyenzo za kazi kazi yao hiyo, ndiyo inawatesa kuingia katika madhara hayo ya kiafya, hata kuhatarisha afya zao kimaisha.

### VIONGOZI MKOA

Martha Mkupas, ni Mkuu wa Wilaya ya Mbogwe, anaunga mkono mradi huo unaolenga kuwasaidia wachimbaji wadogo madini ya dhahabu, waondokane na kukamata zebaki ambayo ni hatari kwa afya zao.

Anawaelimisha wachimbaji kwa kauli: "Lengo la kampuni ni kuwasaidia wachimbaji wadogo wa madini ya dhahabu waondokane na uchimbaji ambao siyo salama kwa afya zao, kutokana na kutumia vifaa duni na kemikali ya zebaki kukamatia dhahabu ambayo siyo salama kiafya."

"Kemikali hii ya zebaki, pia huwa haikamati dhahabu yote bali ni asilimia 30 hadi 40. lakini wakitumia vifaa vya kisasa kukamatia dhahabu kutoka kwenye kampuni hiyo watakuwa wakikamata dhahabu kwa asilimia 100 na hatimaye kuinuka kiuchumi,"anaongeza.

Mkuu wa mkoa wa Geita Robert Gabriel, anasema serikali ya mkoa huo inafurahia kuona kampuni inayotoa msaada kwa vikundi vya wachimbaji wadogo wa madini watakaowapatia vifaa vya kisasa kuendesha shughuli zao, huku wakiwa salama.

AFYA

# Hii ndio maana ya shinikizo la damu, yake yaliyojificha

## • Wengi wagonjwa pasipo kujijua • Ya kuzingatia hata wasioumwa

Na Jackson Paulo

SHINIKIZO la damu ni hali inayomtokea mtu kwa nguvu itokanayo na msukumo wa damu dhidi ya kuta za mishipa ya damu inapokuwa kubwa kupita kiasi. Hiyo ndio inayozaa kinachojulikana kama 'presha'

Kwa kawaida moyo husukuma damu kuelekea sehemu mbalimbali za mwili, hivyo damu inapokuwa inasafiri kwenye mishipa husababisha nguvu ya msukumo yaani 'presha' dhidi ya kuta za mishipa ya damu. Ni kama maji yanavyosafiri kwenye mpira yanapotoka kwenye bomba.

Hali hiyo ni kawaida kwa viumbe wenye damu, hivyo si sahihi kusema mtu ana 'presha' maana presha (nguvu ya msukumo) ni lazima iwepo, kuwezesha damu isafiri na ndio maana kuna baadhi ya maeneo ya mwili kama shingo, mtu anapogusa anauhisi msukumo wa damu.

Kwa maana hiyo, kila mtu ana presha ya damu ila ya kiwango fulani na asiyekuwa na presha ina maana amekwishafariki (hakuna mskumo wa damu).

Kwa hiyo, sahihi ni kusema mtu ana tatizo la presha ya kupanda au presha ipo juu na si 'ana presha.'

Presha ya damu inapimwa kulingana na mambo mawili. Kwanza, ni kiasi cha damu kinachosukumwa kutoka kwenye moyo kwenda maeneo mengine ya mwili.

Pili, kuna uangalizi ya kiwango cha nguvu ya ukinzani 'resistance' damu inachokutana nayo inaposafiri ndani ya mishipa ya damu.

Hiyo ina maana kwamba, kadri kiasi cha damu kilichosukumwa na moyo kwenda kwenye mishipa kinapokuwa kikubwa na kadri mishipa ya damu inavyokuwa mwembamba, ndivyo msukumo au 'presha' unavyozidi kuwa mkubwa.

### VIPIMO

Ili kujua mtu ana tatizo la shinikizo la damu, kipimo maalum hufanyika. Presha ya kiwango cha kawaida huitwa 120/80 mm Hg. Zipo aina kadhaa za presha kulingana na kiwango kinachoonyeshwa na kipimo.

Iwapo presha ya mtu inasoma chini ya 120/80, kitaalamu inayajwa hali ya kawaida; 121-129/chini ya 80 ni presha iliyo juu kidogo.

Pia, inapokuwa 130-139/80-89, ni shinikizo la damu lililo kwenye hatua za awali na inapokuwa katika kiwango zaidi ya 140/90 au zaidi hii ni shinikizo la damu hatua ya juu.

Wataalamu wanasema, iwapo itafika kiwango zaidi ya 180/120 au zaidi, hii ni presha ya juu sana na mtu anapaswa kumwona daktari haraka iwezekanavyo.

Nini maana ya 120/80 mmHg? Namba ya juu yaani 120 huitwa 'systolic blood pressure.' Maana yake ni kiwango cha msukumo 'presha' ambacho damu husababishwa kwenye mishipa ya damu safi moyo unapodunda au kusukuma damu.

Namba ya chini mfano 80, huitwa kitalaamu 'diastolic blood pressure' ikimaanisha kiwango cha msukumo wa damu unaosababisha mishipa ya damu pale moyo unapokuwa umepumzika, yaani kati ya pigo moja la moyo na jingine.



Ilivyo huduma na matibabu ya shinikizo la damu. **PICHA ZOTE: MTANDAO**



> **Mtu anaweza kuwa na tatizo la shinikizo la damu kwa miaka kadhaa bila ya kujitambua au kuwa na dalili yoyote, japo uharibifu kwenye mishipa ya damu unaendelea wakati wote huo.**

### DALILI ZAKE

Mtu anaweza kuwa na tatizo la shinikizo la damu kwa miaka kadhaa bila ya kujitambua au kuwa na dalili yoyote, japo uharibifu kwenye mishipa ya damu unaendelea wakati wote huo.

Kwa maana hiyo, watu wengi huwa na shinikizo la damu bila ya kuonyesha dalili yoyote ile, hata kama kipimo kimesoma kuwa presha ipo juu.

Ni wachache wanaokuwa na tatizo hilo na kuweza kuonyesha dalili kama maumivu ya kichwa, kushindwa kupumua vizuri, uchovu wa kila mara, mapigo yasiyokuwa na mpangilio, matatizo ya kuona vizuri au kutokwa na damu puani.

Katika kulikabili hilo, mtu anapaswa kuhakikisha upimaji presha yake ni jambo endelevu, njia mojwapo muhimu ni kwamba kila mara mtu anapohudhuria hospitali.

Na inapotokea, mtu hujahudhuria hospitali, anaweza kuchukua mbadala wa kufanya kipimo cha presha walau kila baada ya miaka miwili, iwapo ameshafikisha umri wa miaka 18 na zaidi.

Iwapo mtu ana umri zaidi ya miaka 40 au kati ya miaka18 na 39 (lakini yupo kwenye kundi la wenye hatari ya kupata shinikizo la damu), Ahakikishe anafanya kipimo kila mwaka.

Iwapo tayari ana tatizo hilo, ajenge mazoea ya kumuona daktari atakayemshauri afanye kipimo cha klia mara kufuatilia mwenendo wa afya yake.

### KWANINI SHINIKIZO?

Chanzo kamili cha shinikizo la damu hakifahamiki. Lakini, kuna hali au vitu vinavyomfanya mtu kupata tatizo hilo.

Msingi wa chanzo cha shinikizo la damu kimejikita weza kuwa kwenye makundi mawili. Aina ya kwanza huwa ni aina ya msingi yaani 'primary.' Hiyo huhusisha shinikizo la damu lisilokuwa na chanzo maalum, lakini limejijenga mwilini taratibu na kwa kipindi kirefu.

Aina ya pili inaitwa 'secondary' inayosababishwa na hali, kitu au ugonjwa fulani. Baadhi ya vitu au mambo yanayosababisha aina hii ya pili, ni pamoja na matumizi ya tumbaku, unene au uzito uliopitiliza kiwango na kutofanya mazoezi ya mwili.

Pia, kuna matumizi ya chumvi nyingi kwenye chakula, msongo wa mawazo, matumizi makubwa ya vileo, umri mkubwa, tatizo la kurithi, familia au kuwa na historia ya tatizo la shinikizo la damu au tatizo sugu la figo.

Wakati mwingine, ujauzito pia huchangia mtu kupata tatizo la shinikizo la damu la muda mfupi.

### MADHARA YALIVYO

Shinikizo la damu ni hatari kwa sababu husababisha moyo kutumia nguvu kubwa kusukuma damu mwilini, hivyo kuchangia mishipa ya damu safi kuwa migumu zaidi (ili kustahimili msukumo huo).

Presha inapokuwa juu na kwa kipindi kirefu, husababisha madhara mengi kama;shinikizo la moyo; kiharusi 'stroke'; moyo kushindwa kufanya kazi; kuta za mishipa ya damu safi kudhoofika, kutanuka au kuchangia kupasuka.

Aidha, kuna athari za kudhoofu mishipa ya damu kwenye figo kutanuka au kupasuka mishipa ya damu ya kwenye macho na wakati mwingine kupata matatizo ya kumbukumbu.

### NAMNA KUEPUKA

Ili kuepuka uwezekano wa tatizo la shinikizo la damu unapaswa kuepuka mambo niliyotaja hapo juu ambayo husababisa uwezekano wa mtu kuweza kupata tatizo hili.

Baadhi ya mambo hayo ni pamoja na; kuepuka matumizi ya tumbaku, pia matumizi ya pombe kupitiliza, epuka matumizi ya chumvi nyingi kwenye chakula, fanya mazoezi ya mwili imara kila mara, epuka unene au uzito uliopitiliza, pia epuka msongo wa mawazo.

• ***Mwasiliano baruapepe: jacpole@gmail.com***

AFYA

# Namna ulivyo uzazi, idadi ya watu inavyoshuka duniani

• Kusini Jangwa Sahara rekodi yaja, Nigeria 'yawasha taa' kwa mengi




Wakazi wa Nigeria wakiwa katika maandamano yanayowahusu. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

UTAFITI uliochapishwa katika jarida la kitabibu Lancet, unabashiri kushuka uwezo wa uzazi duniani, hapo kukimaanisha kupungua idadi ya watu ifikapo mwishoni wa karne iliyopo.

Aidha, katika baadhi ya nchi zikiwamo za Kusini mwa Jangwa la Sahara, nako kunatarajiwa kutaongezeka wakazi maradufu.

### JAPAN

Kunatarajiwa idadi ya watu kupungua kwa zaidi ya nusu kutoka milioni 128 waliorekodiwa mwaka 2017, hadi chini ya milioni 58 mwishoni mwa karne iliyopo.

Jarida la Lancet linafafanua matarajio ya kuongezeka idadi ya watu wenye umri mkubwa zaidi ya miaka 100 kwa wastani wa asilimia 35, ifikapo mwaka 2040 na wakati huohuo, kutakuwapo uzazi mdogo.

Wastani unaohitajika kwa maendeleo hivi sasa duniani, ni nchi kuwa na wastani kila mtu kuwa na takriban watoto wawili. Katika hilo, Japan iliyokuwa makini dhidi ya wahamiaji, hivi sasa inakuwa ikilegeza sera kwa wahamiaji, ingawa sura ya pili kuna madai ya kunyonywa wafanyakazi wahamiaji.

### ITALIA

Ripoti inataja zaidi ya nusu ya wakazi watapungua, kutoka watu milioni 61 mwaka 2017 hadi milioni 28 mwishoni mwa karne iliyopo.

Utafiti wa Lancet unafafanua kama ilivyo Japan, Italia mwaka

> **Tuna familia nyingi sana ambazo hata haziwezi kuwalisha watoto walionao, ukiacha huduma nzuri za matibabu au hata kuwapatia watoto elimu bora, kwa hiyo ni lazima tuzungumzie mambo haya.**

2019 ilikuwa na wazee wengi. Benki ya Dunia ilibainisha mwisho wa karne wazee wenye zaidi ya miaka 65 watakuwa asilimia 23 ya wakazi wote.

Mwaka 2015, serikali alianzisha kampeni ya kutoa malipo ya Paundi za Kiingereza 725 kwa wanandoa, ambayo ni sawa na zaidi ya Sh. milioni mbili, lengo ni kuinua kiwango cha uzazi nchini humo.

Hadi sasa, Italia ina idadi ndogo ya wakazi katika Muungano wa Ulaya na wakati huohuo, takwimu za mwaka juzi, ilipata wahamiaji 157,000.

### CHINA

Mwaka 1979, China ilianzisha sera ya kuwa na mtoto mmoja. Lengo ni kupunguza kasi ya ongezeko la watu, huku kukiwapo hofu ya athari zinazoweza kutokea katika mipango uchumi.

Hivi sasa ni nchi yenye idadi kubwa zaidi ya wakazi duniani na inakabiliwa na kushuka idadi ya watu wanaoozaa.

Utafiti kutoka taasisi ya Lancet, unabashiri idadi ya watu China itaongezeka kwa kiwango cha juu cha bilioni 1.4 katika kipindi cha miaka minne, kabla ya kuanza kupungua hadi milioni 732 itakapofika mwaka 2100.

Takwimu za nchi hiyo inaeleza mwaka jana, kiwango cha uzazi kilishuka, kuvuka kiwango kilichowahi kushuhudiwa miaka 70 iliyopita.

Pia, kuna hofu ya kuwapo idadi ndogo wenye umri wa kufanya kazi, watakaohitaji kusaidia idadi kubwa ya wazee wastaafu watakaokuwapo.

Ni hofu iliyoifanya serikali ya China mwaka 2015 kusitisha sera ya mtoto mmoja na kuruhusu watu kuzaa watoto wawili. Ni mabadiliko yaliyoongeza viwango vya uzazi. Sera ya mtoto mmoja imeacha uwiano wa kijinsia kwa mujibu wa takwimu za mwaka 2019, wanaume ni wengi kuliko wanawake kwa milioni 30.

Wataalamu wanaeleza kwamba, kulegezwa sheria hakujaenda sambamba na msaada wa nyongeza kwa familia, ikimaanisha wengi hawakuwa na uwezo wa kulea zaidi ya mtoto mmoja.

### IRAN

Taifa la Iran pia linatarajia kushuhudia watu kupungua kwa kiasi kubwa kufikia mwisho wa karne na mageuzi makubwa yameshuhudia ongezeko kubwa la watu baada ya Mapinduzi ya Kiislamu ya Mwaka 1979, ikatekeleza sera ya udhibiti wa uzazi.

Mwezi uliopita, Wizara ya Afya ya nchi hiyo ilitahadharisha kasi ya kushuka idadi ya watu katika kiwango chini ya asilimia moja, haki inayokaribisha idadi kubwa zaidi ya wazee katika miaka 30 ijayo.

Nchini Iran, kunaripotiwa ndoa na watoto imepungua kwa sehemu kubwa kutokana na hali ngumu ya uchumi.

Katika juhudi za kuinua idadi ya watu wake, mwezi uliopita Iran iliamua wanaume hawatofungiwa uzazi(vasectomies) katika vituo vya serikali na dawa za kuzuia mimba zitatolewa kwa wanawake pekee.

### BRAZIL

Brazil imeshuhudia kupungua viwango vya uwezo wa kuzaa miaka 40 iliyopita, kutoka uwezo wastani wa watoto sita kila mwanaume mwaka 1960, hadi wastani wa mtoto mmoja mapaka wawili.

Utafiti wa Lancet unabashiri idadi ya watu Brazil itapungua kutoka milioni 211 kwa mujibu wa hesabu ya mwaka 2017 hadi chini ya watu milioni 164, mwaka 2100.

### INDIA

Utafiti wa kitakwimu unaonyesha India inatarajia kuipata China, nchi yenye idadi kubwa ya watu duniani ifikapo mwaka 2100.

Hiyo inachukua nafasi kwa idadi iliyopo sasa itapungua kutoka bilioni 1.3 bilioni mwaka 2017 hadi chini ya bilioni 1.1 mwishoni mwa karne iliyopo.

Kiwango cha uzazi hivi sasa kiko katika wastani wa watoto wawili hadi watatu (2.24), kutoka watoto watano hadi tisa (5.91) waliozaliwa mwaka 1960.

Waziri Mkuu Narendra Modi, katika wito wake, anatoa wito watu kuwa na familia ndogo, akifafanua: "Kuongezeka idadi kubwa ya watu kutasababisha matatizo mengi kwa kizazi chetu kijacho."

Anawasihi watu kujifunza kutoka kwa wenye familia ndogo na jamii kuielewesha umuhimu huo.

### NIGERIA

Nigeria ni nchi ya barani Afrika yenye wakazi milioni 206 mwaka huu, jarida la Lancet linabashiri itakuwa ya pili kwa idadi kubwa ya watu duniani kufika milioni 791, ifikapo mwisho wa karne iliyopo.

Pia, kunatarajiwa idadi kubwa ya watu wenye umri wa kufanya kazi duniani ifikapo mwaka 2100, huku kukishuhudiwa ongezeko kubwa la pato la ndani ya nchi, kwa wakati huo.

Utafiti mpya wa jarida Lancet, unaeleza wakazi Kusini mwa Jangwa la Sahara, wanatarajiwa kuongezeka mara tatu ya idadi iliyopo sasa na kufika zaidi ya watu bilioni tatu, mwaka 2100.

Waziri wa Fedha wa Nigeria, Zainab Ahmed ana maono:"Tunahitaji kuzungumza juu ya viwango vya uzazi vya Nigeria." Waziri wa Fedha wa Nigeria, Zainab Ahmed, anasema kuna haja ya kuwapo mazungumzo yanayohimiza kuinua kiwango cha uzazi.

"Tuna familia nyingi sana ambazo hata haziwezi kuwalisha watoto walionao, ukiacha huduma nzuri za matibabu au hata kuwapatia watoto elimu bora, kwa hiyo ni lazima tuzungumzie mambo haya," anasema.

***• Kwa mujibu wa taarifa na ripoti tofauti.***





# Asasi zakumbwa na ukosefu wa fedha

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MRATIBU wa Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binadamu Tanzania (THRDC), Onesmo Olengurumwa, amesema mashirika mengi ya kiraia yanakabiliwa na uhaba wa fedha kwa ajili ya kutoa elimu ya mpigakura pamoja na ufuatiliaji wa uchaguzi mkuu 2020.

Olengurumwa aliyasema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari wakati akitoa tamko la hali ya utetezi wa haki za binadamu Kanda ya Kati.

Alisema baadhi ya mashirika yamepata vibali vya uchaguzi lakini hayana rasilimali fedha ambazo zingetumika kwa ajili ya kutoa elimu ya mpiga kura na ufuatilia wa mchakato mzima wa uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

"Mashirika mengi yamepata vibali vya uchaguzi lakini changamoto kubwa ni ukosefu wa rasilimali fedha. Hali hii inaweza kusababisha mashirika machache sana kushiriki katika utoaji wa elimu ya mpigakura na ufuatiliaji wa uchaguzi mkuu mwaka huu," alisema.

Pia alisema kutokana na hali hiyo wadau mbalimbali wanatakiwa kujitokeza kuyawezesha mashirika ili kuyapatia fedha za kuendesha shughuli mbalimbali za uchaguzi mkuu. Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), alisema inatakiwa kutumia mfumo kama ilivyokuwa miaka ya nyuma ya kuyaachia mashirika makubwa kama vile Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kuratibu utoaji wa elimu pamoja na ufuatiliaji wa uchaguzi mkuu.

"Mfumo wa zamani uikuwa unasiidia mashirika makubwa yanapopata fedha yanawezesha yale madogo kupata fedha pia ili kuendesha shughuli mbalimbali za uchaguzi lakini mwaka huu ni ngumu shirika moja moja kupatiwa fedha za uchaguzi," alisema.

Olengurumwa alitoa wito kwa vyombo vya dola nchini kuzipa kipaumbele kesi za ukatili wa kijinsia, zinazoripotiwa na watetezi wa haki za binadamu ili kupunguza wimbo la matukio hayo.

"Tunatoa wito pia kwa watetezi wa haki za binadamu kuwa na mifumo ya ukusanyaji taarifa za matukio ya ukatili wa kijinsia iliyounganishwa na mamlaka kama vile jeshi la polisi," alisema.

Hata hivyo, aliwataka watetezi wa haki za binadamu kutojihusisha na shughuli za kisiasa, ili kuondoa dhana ya kutambulika kama wanasiasa na kutengeneza mgawanyiko na kwa wananchi wenye itikadi tofauti.

Naye Mratibu wa LHRC Mkoa wa Dodoma, William Mtwazi, alisema wanahabari nchini wana wajibu wa kuhamasisha wananchi kushiriki uchaguzi mkuu kwa kuzingatia sheria, utaratibu na msingi iliyowekwa ili amani na utulivu kuendelea kulindwa.



Mfanyabiashara Sanga Mwakaleli, akiandaa fagio la chelewa kwa ajili ya kuuza katika soko kuu la Majengo jijini Dodoma, jana. Fagio moja liliuzwa kwa bei ya 250/-. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Waonywa hatari kuibuka njaa

**Na Ibrahim Joseph,** KONGWA

WANANCHI wametakiwa kutunza chakula cha kutosha kwa ajili ya familia zao na kuacha tamaa ya kuuza ili kuepukana na baa la njaa linaloweza kujitokeza.

Ushauri huo ulitolewa jana na Mkurungenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Kongwa, Dk. Omari Mkulo, alipozungumza na waandishi wa habari.

Dk. Mkulo aliwataka wananchi waliofanikiwa kupata mazao ya kutosha katika msimu huu wa kilimo kuhakikisha wanatunza na kuhifadhi ili kutosheleza kwa ajili ya familia zao na kuepuka kuuza chakula chote.

"Mwaka huu bei ya mazao ipo juu, mkulima asipoangalia anaweza kuuza mazao yote na kuishia kuja kununua chakula hicho kwa bei kubwa zaidi, hivyo ninawataka wananchi kutunza chakula hicho," alisema.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa katika msimu wa mavuno mwaka huu, wilaya hiyo imepata mazao mengi ya chakula na biashara, hivyo wakulima wahakikishe wanahifadhi cha kutosha kwa ajili ya familia zao. Alisema anajua wakulima wengi wanategemea kuuza mazao yao ili kununua mahitaji mengine na kulipa gharama za shule lakini wauze kwa tahadhari ya kubaki na chakula cha familia.

"Wakulima wetu wengi wanategemea kuuza mazao yao kununulia mahitaji kama nguo,ujenzi wa nyumba na kununulia sare kwa ajili ya wanafunzi lakini chakula kinaumuhimu zaidi," alisema.

Alitaja maeneo yaliyofanikiwa kwa kilimo cha mahindi katika msimu wa kilimo mwaka huu kuwa ni Zoisa, Mkoka, Banyibanyi, Kibaigwa, Ngomai na Chitego.

Dk. Mkulo alisema ukanda huo pia umevuna mazao mengi ya biashara kama alizeti, karanga, ufuta na mtama, hivyo mategemeo ni wananchi hao kufanikiwa kiuchumi zaidi na kuiongezea halmashauri mapato.

Hata hivyo, alisema kuna baadhi ya maneo machache ambayo mazao yao yaliharibiwa na mvua kubwa zilizonyesha katika masimu wa mvua wa mwaka huu kwa sababu hiyo watakuwa na upungufu wa chakula .

Pia alisema mafanikio hayo yametokana na halmashauri hiyo kwa kushirikiana na wataalmu wa kilimo na viongozi wengine kuwahamasisha wananchi katika kilimo.

# Kampuni yatoa elimu ya kilimo

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KAMPUNI inayounganisha wakulima na kuwezesha kulima kisasa (JATU PLC) imesema iko tayari kutoa elimu kwa wakulima ili kulima kilimo cha kisasa na chenye tija.

Aidha JATU PLC imemshukuru Rais John Magufuli kwa jitihada alizozifanya hadi kupelekea nchi kufikia uchumi wa kati.

Akizungumza na waandishi wa habari, Meneja wa JATU Plc Kanda, Claudia Simon, alisema pamoja na mambo makubwa aliyoyafanya Rais Magufuli ikiwamo ujenzi wa reli ya kisasa na amekuwa mstari wa mbele katika kuwajali wananchi wenye kipato cha chini wakiwamo wakulima.

Alisema kupitia uchumi wa kati, JATU wapo kwa ajili ya kuwasidia wakulima mbalimbali kwa kuwapa elimu bora ya namna ya kufanya kilimo chenye tija.

"Tunafanya kilimo shirikishi kwa wanachama kwa kuwatafutia mashamba na kuyalima katika mikoa mbalimbali kwa kuzingatia aina ya udongo iliyoko shambani na zao linalotakiwa. Lakini pia mazao yakiwa tayari sisi wenyewe tunayanunua kwa bei elekezi ya serikali kwa wakati huo," alisema.

Alisema wamekuwa wakiwafikia wakulima katika mikoa mbalimbali, lengo likiwa ni kutoa elimu ya namna ya kulima kisasa.

Pia alisema wamekuwa wakilima katika mikoa kama ya Morogoro, Manyara ,Dodoma, na Njombe

Mmoja wa wanufaika wa JATU, Faraja Mwakifuna, alisema kabla hajajiunga na kampuni hiyo, alishawishika kutoka kwa rafiki yake ambaye alilima na kupata magunia 25 ya mpunga wilayani Kilombero.

"Nilipoona mafanikio aliyoyapata rafiki yangu, nami nilijiunga na JATU. Nimelima ekari nne za mpunga na Mungu akijaalia nataka nilime ekali 40," alisema.

Aidha, alisema kampuni ilimkopesha na kulima huku akiwa ofisini na bila makato yoyote.





# TARI yakamilisha utafiti kufufua ulezi

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI) Kituo cha Uyole, Mbeya imekamilisha utafiti wa kufufua zao la ulezi ambalo linadaiwa kuwa hatarini kutoweka kutokana na uzalishaji wake kupungua nchini.

Licha ya kuzalishwa kwa kiwango kidogo, zao hilo linadaiwa kuwa na faida kubwa kiuchumi, huku wataalamu wakidai lina virutubisho vingi kwa afya ya binadamu kuliko mazao mengine ya nafaka.

Zao hilo, asili yake inadaiwa kuwa ni Afrika Mashariki ambako limekuwa likilimwa kwa miaka mingi, lakini katika miaka ya karibuni kilimo cha ulezi kimeshuka kiasi kikubwa.

Kutokana na zao hilo kuwa katika hatari ya kutoweka, wataalamu wa TARI Kituo cha Uyole wameamua kuchukua hatua za kulinusuru na kuhamasisha kuongeza uzalishaji kwa faida ya wakulima na taifa kwa ujumla.

Mtafiti mwandamizi wa mazao ya mpunga na ulezi, Dk. Denis Tippe, alisema ili kulifufua zao hilo wamekuja na mkakati wa kusambaza aina tatu za mbegu ambazo zitalimwa maeneo yote nchini.

"Zao la ulezi lina faida kubwa kwa afya ya binadamu kuliko mazao mengine ya nafaka, kwa vile lina madini mengi ya Zinc, chuma na virutubisho vingine vinavyopatikana kwa wingi kuliko kwenye mazao mengine ya nafaka," alisema Dk. Tippe.

Alisema Watanzania wamekuwa na jadi ya kutumia ulezi kwa kusaga na kupata unga ambao huutumia kwa kupika uji, ugali, vitafunwa na aina mbalimbali za vilevi, hali ambayo inafanya zao hilo kuwa muhimu zaidi.

Mkurugenzi wa TARI Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, alisema wamekamilisha utafiti huo na kupata aina tatu za mbegu bora za ulezi zenye uwezo wa kutoa mazao mengi na kuleta faida kubwa kwa wakulima wa zao hilo. Alisema mbegu hizo tayari zimeanza kusambazwa maeneo mbalimbali nchini na kwamba zitapandwa kulingana na aina ya udongo uliopo katika eneo husika, kwa lengo la kuongeza mavuno kutoka magunia sita kwa ekari 40.

Ofisa wa Uhawilishaji wa Teknolojia kutoka TARI Uyole, Rehema Ole-Seenga, alisema mbali na zao hilo, taasisi hiyo pia imefanya utafiti wa mazao mengine mengi ambayo pia yanamsaidia mkulima kujikwamua na umaskini.




Katibu Mkuu Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya (kulia), akikabidhi magunia 20 ya mpunga kwa Rais wa Serikali ya Wanafunzi wa Chuo cha Kilimo Uyole, Baitan Sanga, katika hafla iliyofanyika chuoni hapo, mkoani Mbeya juzi, ikiwa ni utekelezaji wa ahadi yake aliyoitoa kwa wanafunzi wakati wizara yake mkoani Mbeya hivi karibuni. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wenye ulemavu wahamasishwa kuchangamkia kugombea ubunge

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MWENYEKITI wa Chama cha Viziwi Tanzania (CHAVITA) Mkoa wa Mbeya, Tusekile Mwalwega, amehamasisha kundi hilo hususani wanawake kujitokeza kwenye kinyang'anyiro cha kugombea nafasi ya ubunge wa viti maalum mkoani humo.

Mwalwega alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na Nipashe kuhusu maandalizi ya kundi hilo kuwania nafasi ya ubunge wa viti maalum Mkoa wa Mbeya.

Alisema kipindi hiki kundi la viziwi walijitokeza kwa wingi kuwania nafasi hiyo kuchukua fomu kuomba ridhaa ya kuchaguliwa kupitia kundi maalum la watu wenye ulemavu.

"Hadi sasa watu wawili pekee wamejitokeza kuchukua fomu ili kuomba nafasi ya kuchaguliwa nafasi ya viti maalum kupitia kundi la watu wenye ulemavu tulitamani wengi wajitokeze, lakini kikwazo kikubwa ni uhaba wa wakalimani wa lugha ya alama lakini ukata wa fedha za kuchukulia fomu," alisema Mwalwega.

Mmoja wa watia nia nafasi ya ubunge viti maalum kupitia kundi la viziwi, Lupi Mwaisaka, alipongeza utaratibu wa namna ya uchukuaji fomu kwa kushirikisha makundi yote.

Alisema miongoni mwa sababu zilizomsukuma kuomba ridhaa ya nafasi ya ubunge wa viti maalum Mkoa wa Mbeya ni kutetea haki za watu wenye ulemavu ikiwamo kujengewe miundombinu rafiki ya kupatia huduma kwenye taasisi za umma.

Sambamba na nia yake, Mwaisaka alimpongeza Rais John Magufuli kwa kuwapa nafasi watu wenye ulemavu kwenye uteuzi mbalimbali kutokana na suala hilo alisema wataendelea kumuunga mkono kwa kujitokeza kwenye nafasi za uongozi kipindi hiki cha uchaguzi.

Aliwaomba wana Mbeya kumwamini na kumpa ridhaa ya kuibuka kidedea katika nafasi hiyo ili kuliwakilisha kundi hilo bungeni kwa kuhakikisha anatetea haki za wananchi wote wakiwamo wenye ulemavu.

## Vyuo vya kilimo vyatupiwa jicho

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI inakusudia kuanzisha vyuo vipya vya elimu ya kilimo na kuongeza kozi za masomo hayo kwenye vyuo vikuu vilivyopo ili kuwawezesha wanafunzi wanaohitimu kupata nafasi ya kuendelea na elimu ya juu.

Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo, Gerald Kusaya, aliyasema hayo juzi wakati akizungumza na wanafunzi wa Chuo cha Kilimo Uyole mkoani hapa.

Kusaya alisema serikali imebaini kuwa kuna mahitaji makubwa ya vyuo vya kilimo vya elimu ya juu nchini na tayari imeshaanza kuchukua hatua kukidhi mahitaji hayo.

"Hivi sasa tuna chuo kimoja tu kinachotoa elimu ya juu ya kilimo ambacho ni Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) kilichoko mkoani Morogoro, lakini serikali inakusudia kuanzisha vyuo vingine vipya kwa sababu inaona mahitaji ya elimu hiyo yanazidi kuwa makubwa nchini," alisema Kusaya.

Alisema kabla ya kukamilisha mipango ya kufungua vyuo vipya, serikali imeanzisha kozi za kilimo kwenye baadhi ya vyuo vikuu vya serikali, ili kukabiliana na wimbi kubwa la vijana wanaohitimu katika vyuo vya kati vya kilimo.

"Tayari serikali imeshaanzisha kozi za kilimo katika Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Chuo Kikuu cha Mandela, lakini Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine nacho kimeanza kufungua matawi yake katika maeneo mengine mbalimbali nchini kwa nia hiyo hiyo ya kuwasaidia vijana kupata elimu ya juu ya kilimo," alisema Kusaya.

Hivi sasa kuna vyuo vya kilimo vya kati 14 vinavyotoa elimu katika ngazi ya stashahada (diploma) na wahitimu wote wanategemea chuo kimoja tu cha SUA kupata elimu ya juu.

Mkurugenzi wa Mazao kutoka Wizara ya Kilimo, Nyasebwa Chimagu, alisema ili kupata wataalamu bora wa kilimo, wizara imeanzisha dawati linaloratibu uendelezaji wa kilimo kwa kuwashirikisha vijana ili kuwawezesha kupata mafunzo kwa vitendo.

Chimagu alisema dawati hilo pia liwasaidia vijana kupata mikopo nafuu kwa ajili ya kufungua miradi ya kilimo kwa lengo la kufanya mafunzo ya vitendo.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Godfrey Mkamilo, alisema utafiti wa kilimo ndiyo nyenzo muhimu ya kuongeza uzalishaji wa mazao hivyo ni muhimu vijana wakajikita kwenye mafunzo ya utafiti wa kilimo.







Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Dk. Idrisa Muslim Hija (wa tatu kulia), akitoa maelekezo ya matengenezo ya majengo ya maabara za sayansi, wakati alipofanya ziara ya kuzikagua zilizojengwa na kampuni ya Salim Constructors Ltd, Wilaya ya Kati Kusini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Biashara ya binadamu inavyowapa mateso waathirika

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Kazi, Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Maendeleo ya Wazee, Wanawake na Watoto, Maua Makame Rajab, amesema kuwa kushamiri kwa biashara haramu ya usafirishaji binadamu ni mateso makubwa kwa waathirika wa biashara hiyo.

Alisema mateso hayo ni kupigwa, kubakwa, kunyimwa chakula, kufanyishwa kazi bila malipo, kuuzwa kwa waajiri zaidi ya mmoja na kufanyishwa kazi bila ya malipo.

Aliyaeleza hayo wakati akifungua mafunzo kwa waandishi wa habari kuhusu kupinga biashara haramu ya usafirishaji binadamu yaliofanyika mjini hapa.

Alisema waathirika hao pia kupata mateso hadi kufariki dunia hali ambayo iliyolazimu Umoja wa Mataifa kuandaa na kuridhia itifaki ya kimataifa ili kuzuia na kupinga usafirishaji haramu wa binadamu.

Alisema Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilisaini itifaki hiyo mwaka 2000 na kuiridhia mwaka 2006 kuzuia na kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Alisema licha ya Tanzania kuridhia sheria hiyo, lakini bado haijaanza kutekelezwa na tararibu zinaendelea ili ianze kutekelezwa. "Sheria hii kimsingi kama ilivyo ile ya kimataifa, inaharamisha matendo yote yanayohusiana na uhalifu wa usafirishaji wa binadamu na pia inazungumzia jinsi ya kuwalinda wahanga," alisema.

Vile vile, alisema usimamizi wa utekelezaji wa sheria uko mikononi mwa kamati ya kitaifa ya kuzuia na kupambana na biashara haramu ya usafirishaji wa binadamu.

Alisema Serikali ya Zanzibar inaungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Kupinga Biashara Haramu ya Usafirishaji wa Binadamu.

Pia, alisema serikali ina dhamira ya kuendelea kuifanya nchi kuwa ya viwanda na uchumi wa kati.

Lengo hilo litafikiwa ikiwa kuna rasilimali watu wenye nguvu za uzalishaji na ujuzi hasa vijana. Alisema moja ya matokeo mabaya ya biashara hiyo ni uondoaji wa rasilimali watu ambao ni wazalishaji. Naye Mwenyekiti wa kamati ya kuzuia biashara haramu ya binadamu, Adatus Magere, alisema wahalifu 61 wa usafirishaji haramu wa binadamu Tanzania wamehukumiwa kwa mwaka 2015 hadi 2020. Alisema kati ya hao 12 wapo gerezani na waathirika 577 wameokolewa.

Alisema biashara hiyo isipodhibitiwa ni hatari kwa usalama wa wananchi.

# Afariki dunia kwa kuteketea kwa moto

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

HIJA Suleiman (38), mkazi wa Mwera amefariki dunia katika ajali ya moto.

Akizungumza na vyombo vya habari, Kaimu Kamanda Mkoa wa Mjini Magharibi, Simon Pasua, alisema ajali hiyo ilitokea juzi majira ya saa 8:00 mchana katika kituo cha mafuta depoti ya PUMA Mtoni, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja.

Alisema, marehemu huyo ni dereva wa kampuni ya Bachu na chanzo cha moto huo kilitokana na gari iliyokuwa ikiweka mafuta ya taa katika tangi kulipuka.

Alisema Jeshi la Polisi lilishirikiana na Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kuhakikisha inadhibiti moto huo na hauendelei kuleta madhara.

Kaimu Pasua alisema Jeshi la Polisi linaendelea na upelelezi wa tukio hilo na mwili wa marehemu umeshapelekwa katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja kwa uchunguzi.

"Hivi sasa bado mapema kueleza chanzo cha tukio hili tunaendelea na upelelezi, lakini moto umedhibitiwa na eneo lililolipuka limefungwa," alisema.

Naye Kamishna wa Kikosi cha Zimamoto na Uokozi Zanzibar, Mwalim Abdalla Ussi, alisema kikosi hicho kimefika kwa wakati na kuudhibiti moto huo ili usiendelee kuleta madhara.

"Tunashukuru tumefika katika muda muafaka na moto huu ulisababishwa na mafuta ya taa na ingekuwa petroli maafa yangekuwa makubwa," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Mtendaji Kamisheni ya kukabiliana na maafa Zanzibar, Makame Khatib Makame, alisema tathmini halisi ya tukio bado haijajulikana na kukipongeza kikosi KZU kwa kuudhibiti moto huo na kuepusha maafa.

Aliziomba kampuni zinazosimamia maeneo hayo kuweka mifumo madhubuti ya kuzuia majanga yatakapojitokeza.

Naye Mkuu wa Wilaya ya Magharibi 'A' ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi na Usalama, alisifu juhudi zilizochukuliwa na kikosi hicho na kuwatoa hofu wananchi wa janga lililotokea.

# Wizara yagoma kusaini fomu ya makabidhiano majengo

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WIZARA ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, imekataa kusaini fomu ya makabidhiano ya majengo yalio chini ya Mkandarasi Salim Constructors Ltd., yaliopo Wilaya ya Kati na Mkoa wa Kusini Unguja kutokana na kutomalizika kwa baadhi ya miundombinu yake.

Naibu Katibu Mkuu wa wizara hiyo, Abdallah Mzee Abdallah, alisema utaratibu wa wizara yake kupokea majengo yakiwa yamekamilika katika miundombinu yote kama mkataba utavyoeleza.

Akizungumza katika majumuisho ya ziara ya kuangalia majengo ya maabara za kisayansi kwa shule nne zinazosimamiwa na mkandarasi huyo, alisema makubaliano yao ni kukabidhiana majengo yote na endapo jengo moja litakuwa na kasoro hawatoweza kusaini fomu ya makabidhiano ya kumaliza majengo.

Alisema katika ziara yao wameona kuwapo tatizo la umeme katika maabara ya Uroa hali inayosababisha kushindwa kukagua mifumo yote ya umeme pamoja na maabara ambayo ndio huduma muhimu katika mazingira ya shule hizo.

Alisema ili taifa lizalishe wasomi hasa wa masomo ya sayansi ipo haja ya kuboresha miundombinu bora ya kielimu kuanzia majengo pamoja na maabara za kutosha.

Aliwahimiza makandarasi kufanya marekebisho yaliyojitokeza katika majengo hayo kwa wakati waliokubaliana.

Naye Mkurugenzi wa Idara ya Mipango Sera, Khalid Masoud Waziri, alisema lengo la ziara hiyo ni kuhakikisha majengo yote ya mradi wa ujenzi wa maabara za kisayansi yanakamilika kwa kiwango imara na salama kwa ajili matumizi ya watoto shuleni.

Kwa upande wake mshauri elekezi wa mradi huo, Casmil Ntobangi, alisema ukosefu wa mchanga, mvua kubwa na mlipuko wa maradhi ya Covid-19 imesababisha kuchelewa kukamilika kwa wakati maabara hizo na kumtaka mkandarasi kuhakikisha wanamaliza matengenezo hayo.

Katika ziara hiyo wamefanikiwa kukagua maabara za Regeza Mwendo, Bwejuu, Uroa na Unguja ukuu ambazo zimejengwa chini ya ufadhili wa mradi wa ZISP na jumla ya maabara za kisayansi 24 zimejengwa Unguja na Pemba na ufadhili wa mradi huo.

HABARI KIMATAIFA

# Corona yaahirisha kesi ya Al Bashir

**KHARTOUM,** Sudan

KESI dhidi ya Rais wa zamani wa Sudan, Omar Hassan al Bashir, imeahirishwa kutokana na hofu ya ugonjwa wa corona na kukosekana kwa hatua za kuzuia maambukizi ya ugonjwa huo mahakamani.

Watu wengi walikuwa wamekusanyika katika Mahakama ya Mji Mkuu wa Sudan, Khartoum, ambako Bashir mwenye tabasamu usoni, mwenye afya nzuri alikuwa amepandishwa kizimbani akiwa amevalia vazi refu la utamaduni wa Wasudan la Jalabiyya.

Jaji wa mahakama hiyo alisema kutokana na watu kujaa sana katika chumba cha mahakama, hali ambayo hairuhusu uzingatiaji wa umbali unaotakiwa wa watu kutokaribiana kwa mujibu wa hatua za kudhibiti kuenea kwa ugonjwa wa corona, kesi dhidi ya Bashir imeahirishwa na itasikilizwa tena Agosti 11, mwaka huu.

Al Moaz Hadra mmoja wa mawakili waliowasilisha kesi hiyo mahakamani ameliambia Shirika la Habari la Ujerumani (DPA) kwamba Bashir anakabiliwa na mashtaka ya kukiuka katiba, kuvunja sheria kuhusu majeshi na uasi.

Wakili Hadra aidha amesema: "Kesi hii ni onyo kwa mtu yeyote, awe anatokea katika ulingo wa siasa au jeshini, anayejaribu kuharibu mfumo wa katiba. Hiki ni kitendo cha kihalifu kwa mujibu wa sheria. Tutalinda demokrasia ya Sudan kupitia kesi hizi."

Hashem al-Gali, mmoja wa mawakili 150 wa upande wa utetezi alilalamika kuhusu kesi dhidi ya Bashir akisema ni mchezo mchafu wa siasa unaofanywa.

"Hii ni kesi ya kisiasa ambayo inaendeshwa kwa kisingizio cha sheria kama kesi halali. Ni kesi ya kisiasa inayofanyika katika mazingira ya ukatili kwa upande wa mfumo wa mahakama na upande wa utetezi," alisema Hashem al-Gali.

Alisema kesi dhidi ya Bashir inalilenga vuguvu la kiislamu na lengo lake kubwa ni kulionyesha vuguvugu hilo kama la kigaidi.

Bashir, mwenye umri wa miaka 76 atapandishwa kizimbani pamoja na washtakiwa wengine kadhaa, wakiwamo makamu wa rais wawili wa zamani pamoja na mawaziri na magavana wa zamani.

Iwapo atatiwa hatiani Bashir, ambaye tayari anatumikia kifungo kwa ufisadi, huenda akakabiliwa na hukumu ya kifo.

Al Bashir aliingia madarakani mnamo mwaka 1989 baada ya kuongoza mapinduzi ya kijeshi dhidi ya Waziri Mkuu aliyechaguliwa kwa njia ya demokrasia Sadek al-Mahdi.

Aliondolewa madarakani mnamo Aprili, 2019 kufuatia migomo na maandamano ya barabarani ya kudai demokrasia. **DW**

# Madagascar yaomba msaada kukabiliana ugonjwa corona

**ANTANANARIVO,** Madagascar

WIZARA ya Afya nchini Madagascar imetuma ombi la msaada wa dharura kwa mashirika na taasisi za afya kukabiliana na mlipuko wa ugonjwa wa corona wakati idadi ya wagonjwa ikiongezeka.

Imesema kwamba ugonjwa huo katika wiki za hivi karibuni umesambaa kwa kiwango cha juu nchini Madagascar, huku maeneo kadhaa yakirekodi milipuko hususani mji mkuu wa Antananrivo, kulingana na mtandao wa Actu Orange.

Kumekuwa na ripoti kwamba hospitali za umma nchini Madagascar zimejaa na zimekuwa zikiwalaza wagonjwa walio katika hali mbaya zaidi.

Taifa hilo kwa sasa lina takriban wagonjwa 7,000 wa ugonjwa wa virusi vya corona.

Rais Andry Rajaolina mapema mwezi huu aliweka masharti ya kutotoka nje katika Mji mkuu wa Antananarivo kufuatia kuongezeka kwa maradhi hayo.

**Ni kweli kwamba nimewasiliana na walioambukizwa. Nimeingia katika hospitali zinazowatibu wagonjwa wa corona.**

Mnamo Aprili, mwaka huu Rais Rajaolina alizindua dawa ya mitishamba ya maradhi ya ugonjwa wa corona ambayo ilisambazwa nchini humo. Mizigo kadhaa ya dawa hiyo ya corona pia ilitumwa kwa makumi ya mataifa barani Afrika.

Hata hivyo, uwezo wa kinywaji hicho umepuuzwa na wataalamu wa afya nchini Nigeria na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) mataifa ambayo yalifanyia majaribio dawa hiyo.

Katikati ya Julai Rais wa taifa hilo alitangaza kwamba wabunge wawili wamefariki kutokana na virusi vya corona, huku wengine 25 wakiambukizwa virusi hivyo tangu kisa cha kwanza kilipothibitishwa katika kisiwa hicho mnamo Machi.

Rais Rajoleina pia alisema kwamba yeye na familia yake wamekuwa wakinywa dawa ya mitishamba ya corona inayodaiwa kutibu virusi hivyo ambayo ilizinduliwa Aprili, licha ya onyo kutoka kwa Shirika la Afya Duniani (WHO) kwamba haijaidhinishwa kutumika.

Ni kweli kwamba nimewasiliana na walioambukizwa. Nimeingia katika hospitali zinazowatibu wagonjwa wa corona. Niko salama," alisema Rais Rajoleina na kuongeza:

"Sina virusi vya corona hata kidogo. Sina dalili. Namshukuru Mungu. Nafuata maagizo niliojiwekea, lakini zaidi ya yote mimi na wapenzi wangu mke wangu na watoto wangu, tunakunywa na kufuata maagizo ya dawa yetu ya mitishamba." **BBC**



Mwanamama nchini Uganda akiwa sokoni akiuza bidhaa zake baada ya Rais Yoweri Museveni kutoa ruhusa ya kuendelea kwa shughuli za biashara nchini humo. **PICHA: AFP**

# Wezi waiba sampuli za corona

**JOHANESSBURG,** Afrika Kusini

JESHI la Polisi nchini Afrika Kusini wanachunguza wizi wa lori lililokuwa limebeba sampuli za wagonjwa wa virusi vya corona katika mji wa Port Elizabeth Jumatatu.

Sampuli hizo zinaripotiwa kupotea. Zilikuwa zimewekwa ndani ya maboksi yaliyokuwa yamejazwa barafu.

Maofisa wa afya nchini humo wamewaonya wa walioiba sampuli hizo pamoja na umma wasiziguse kwa sababu zina uwezekano mkubwa wa kuwa na maambukizi.

"Mtu yeyote ambaye ataliona kasha hilo jeupe anatakiwa kuripoti kwa polisi. Tumetoa onyo hilo ili kuhakikisha kuwa kila mtu ana ufahamu. Tunafuraha kwamba suala hili linachunguzwa. Tunashirikiana na mashirika yote na taasisi za serikali katika sekta ya afya kukabiliana na changamoto kama hizi huku tukisonga mbele," ilieleza taarifa kutoka Jeshi la Polisi.

Maofisa wanachunguza idadi ya sampuli zilizoibwa kabla ya kubaini ni watu wangapi watakaopimwa tena, imeripoti tovuti hiyo.

Lori hilo liliibiwa katika eneo la kuegesha magari la kliniki na kutelekezwa muda mfupi baadaye, kulingana na taarifa iliyotolewa na Shirika la habari la Afrika Kusini SABC.

Tayari watu wapatao milioni 2.5 wamefanyiwa vipimo vya virusi vya corona nchini Afrika Kusini. Kwa sasa kuna watu 871 waliofariki kutokana na corona mashariki mwa Cape huku idadi ya wagonjwa ikifikia 65,316.

Nchi hiyo ina idadi ya juu zaidi ya watu walioithibitishwa kuwa na maambukizi ya corona barani Afrika. **BBC**

# SOLSKJAER KUFANYA MAAMUZI MAGUMU KWA DE GEA




**MANCHESTER,** England

OLE Gunnar Solskjaer amesisitiza alikuwa tayari kufanya maamuzi magumu pale Manchester United huku kukiwa na sitofahamu juu ya majaliwa ya David de Gea.

Kiwango cha De Gea kwa mara nyingine kilizua mjadala baada ya golikipa huyo kufanya makosa mawili na kuigharimu United iliyochezea kichapo cha 3-1 kwenye nusu fainali ya kombe la FA kutoka kwa Chelsea, Jumapili.

Kuelekea mchezo wa jana Jumatano dhidi ya West Ham, Solskjaer amesema alijiandaa kufanya maamuzi magumu hapo United.

"Kila maamuzi ni makubwa hapa, hivyo unatakiwa kufanya kile kilichokuwa sawa kwa timu na klabu," alisema kocha huyo wa United akiviambia vyombo vya habari vya Uingereza.

"Tutafanya hivyo Jumapili na wakati msimu utakapokamilika tutafanya maamuzi zaidi."

De Gea amecheza kila dakika kwa United kwenye Ligi Kuu na wapo nafasi ya tano kwenye msimamo huku zikiwa zimesalia mechi mbili mpira kumalizika.




# Ibrahimovic hajui hatima yake

**MILAN,** Italia

ZLATAN Ibrahimovic bado hana uhakika kuhusu majaliwa yake AC Milan huku zikiwa zimebakia mechi mbili tu kumalizika kwa msimu huu.

Straika nyota huyo mwenye umri wa miaka 38, amefunga mabao mawili wakati Milan wakiwafunga 2-1 Sassuolo iliyokuwa na wachezaji 10 uwanjani kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Jumanne.

Wakati mkataba wa Ibrahimovic pale Milan unamalizika mwishoni mwa msimu huu, klabu hiyo ilitangaza Jumanne kuongeza mkataba wa kocha wake mkuu, Stefano Pioli hadi mwaka 2022.

Ibrahimovic, akizungumza baada ya tangazo hilo la Pioli, alisema hana uhakika kuhusu majaliwa yake.

"Bado tuna mechi tatu, bado siku 10, hakuna yoyote aliyesema chochote kwangu na sitarajii chochote kile," alisema kupitia Sky Sport Italia. "Kuna mambo ambayo hayapo kwenye maamuzi yangu, lakini hilo linaonekana kuwa geni kwa upande wangu, lakini tunafanya vizuri vikubwa.

"Tunacheza kwa kujiamini na tumaanini tunaweza kufanya chochote tunacheza kwa kujiamini na tunaamini tunaweza kufanya hivyo."

Milan haijafungwa katika mechi 10 tangu kurudi kwa msimu huu baada ya kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona, na wapo nafasi ya tano kwenye msimamo.

Ibrahimovic, ambaye amefunga mabao nane katika mechi 17 msimu huu, amesifia kiwango cha Milan.

# Klopp: Ubingwa wa Liverpool ni historia

**LIVERPOOL,** England

JURGEN Klopp anaamini ushindi wa Liverpool wa Ligi Kuu msimu huuu "ni moja ya habari kubwa kwenye historia ya soka."

Liverpool hatimaye walimaliza ukame wa miaka 30 na kulitwaa taji la Ligi Kuu mwaka huu ikiwa ni mara ya kwanza tangu mwaka 1990.

Klopp, ambaye alishinda taji la Ligi ya Mabingwa Ulaya, klabu bingwa ya dunia na UEFA Super, anaamini mafanikio hayo yanabakia kuwa kwenye historia ya klabu hiyo.

"Mara zote nilikuwa naona ni jambo zuri kushinda taji la Ligi Kuu kuliko kwenye kwenye fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya," amesema Klopp akinukuliwa na vyombo vya habari vya Uingereza.

"Sasa tumeshinda taji la ligi zikiwa zimesalia mechi saba kabla ya msimu kumalizika, kitu ambacho kinahamasisha.

"Kwa asilimia 100 namna tulivyoshinda taji la Ligi Kuu ni historia bora zaidi kwenye klabu nzima. Nafikiri ni moja ya habari kubwa zaidi katika historia ya soka."



# Arteta: Naungwa mkono asilimia 100 na Kroenke

**LONDON,** England

MIKEL Arteta amewataka mashabiki wa Arsenal kutuliza shutuma zao kwa mmiliki wa klabu hiyo, Kroenke, akisisitiza kwamba, anaungwa mkono na bodi ya klabu hiyo.

Arteta amewaongoza washikabunduki hao kwenye fainali ya kombe la FA baada ya kuwasili katikati ya msimu huu klabuni hapo akitokea Manchester City, lakini kikosi chake kinaweza kumaliza si zaidi ya nafasi ya nane kwenye msimamo wa Ligi Kuu baada ya kupoteza kwa Aston Villa, Jumanne.


Kuelekea mchezo huo pale kwenye uwanja wa Villa Park kulikuwa na bango kubwa lililokuwa likipeperusha angani kutoka kwa mashabiki wa Arsenal likiwa na maneno: "Muunge mkono Arteta, Kroenke aondoke."

Baada ya mchezo huo, kocha huyo aliwaambia waandishi wa habari kwamba anaungwa mkono kwa asilimia 100 na bodi ya klabu hiyo pamoja na Kroenke.

"Hapana, hapana, hapana," alisema Arteta akiiambia Sky Sports. "Kroenke, bodi na mkurugenzi wa michezo, wananiunga mkono kwa asilimia zote.

"Hatujui mambo mengi, tunatakiwa kusubiri kwa muda. Lakini sapoti na kuungwa mkono ni asilimia 100, naamini hilo.

"Mashabiki wanatakiwa kuamini kile ninachokisema. Kama sio kweli nisingesema hivi."






# GREALISH: SIJUI KAMA NITACHEZA ASTON VILLA MSIMU UJAO

**LONDON** England

JACK Grealish ambaye amekuwa akihusishwa na Manchester United - amebainisha kwamba "hana uhakika" kama amecheza mechi yake ya mwisho nyumbani kwa Aston Villa.

Nahodha huyo wa Villa, Grealish aliiongoza timu yake kuibuka na ushindi wa 1-0 nyumbani dhidi ya Arsenal, Jumanne na kukifanya kikosi hicho cha kocha, Dean Smith kuwa juu ya Watford na kutoka kwenye eneo la hatari la kushuka daraja kwenye Ligi Kuu.

Licha ya matokeo ya sasa ya klabu yake hiyo, majaliwa ya kiungo huyo bado hayajulikani.

United imekuwa ni miongoni mwa klabu inayoonekana kunyemelea saini ya Grealish, ambaye hakuweza kuthibitisha kama atakuwa tena kwenye jezi ya Villa msimu ujao.

"Kwa wakati huu sina uhakika," alisema akiiambia Sky Sports. "Nina lengo moja kwamba kuibakiza klabu hii kwenye Ligi Kuu.

"Klabu yote, mashabiki wote wanajua nini ambacho tunakitaka. Hilo ndio pekee ninalolifikiria kwa sasa, kuibakisha klabu hii kwenye Ligi Kuu. Kwa matumaini makubwa tunaweza kufanya hivyo Jumapili na tunapigania kubakia kwenye Ligi Kuu."

# *Aubameyang asubiria ofa ya Barca*

**LONDON,** England

NYOTA Pierre-Emerick Aubameyang bado anaisubiria ofa kutoka kwa Barcelona, ambao walionyesha nia ya kutaka kumsajili wakati huu wa dirisha la majira ya joto, kwa mujibu wa Sky Sport and Sport.

Majaliwa ya Aubameyang pale Arsenal bado hayajulikani, huku mkataba wa fowadi huyo ukiwa unamalizika mwakani.

Aubameyang sasa anajiandaa kusubiria ofa kutoka kwa Barcelona ambao wametajwa kwamba wanawania kumsajili mfungaji huyo wa Arsenal ambaye kwa sasa yupo kwenye kiwango cha kuvutia zaidi.

Nyota huyo wa kimataifa wa Gabon mazungumzo yake ya kusaini mkataba mpya na klabu hiyo yamesimama, huku kukiwa na taarifa kwamba nyota huyo anaondoka klabuni hapo.

Gazeti la Mundo Deportivo limeripoti kwamba straika huyo mwenye umri wa miaka 31 anachukuliwa kama chaguo namba moja kwa Barca kama watashindwa kumsajili nyota wa Inter Milan, Lautaro Martinez.

Aubameyang amefunga mabao 25 katika mechi 42 alizoichezea Arsenal msimu huu.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: NITABAKI PSG MSIMU UJAO

**Asema bila kujali lolote, ataendelea kuwa sehemu ya timu kwa ajili ya kuleta...**

**PARIS,** Ufaransa

KYLIAN Mbappe amesema atakuwa mchezaji wa Paris Saint-Germain msimu ujao "bila kujali lolote."

**Mshindi huyo wa Kombe la Dunia na Ufaransa ameendelea kuhusishwa na mpango wa kuondoka PSG, klabu ambayo alijiunga nayo kutoka Monaco mwaka 2017 awali ikiwa kwa mkopo na kufuatiwa na ada ya euro milioni 180.**

Mbappe alifunga mabao 30 katika mashindano yote kabla ya msimamo wa Ligue 1 kufutwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Fowadi huyo wa Ufaransa atapata nafasi ya kuongeza taji la Coupe de France, Coupe de la Ligue na Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa wiki zijazo, na atabakia pale Parc des Princes msimu wa 2020-21.

"Nipo hapa. Nipo kwenye mradi huu kwa mwaka wa nne," amesema Mbappe akiiambia beIN SPORTS.

"Mwaka wa 50 wa klabu ni mwaka muhimu kwa klabu, mashabiki na kila mmoja, hivyo nitakuwa hapa bila kujali lolote. "Nitajaribu kuleta mataji hapa pamoja na timu na kujaribu kucheza kwa ubora wangu wote mimi mwenyewe."

Mbappe anaweza kuendelea kubakia kuwa mchezaji muhimu zaidi pale Paris, baada ya Thomas Tuchel kubainisha kwamba majaliwa ya Thiago Silva bado hayajajulikana.

PSG ilitangaza nahodha wake huyo anaweza kuondoka mwishoni mwa msimu huu, lakini baadaye ikathibitisha kumwongezea mkataba kwa ajili ya mechi tatu za mashindano yaliyobaki.

Akizungumza kuhusu Silva baada ya ushindi wa mabao 4-0 kwenye mchezo wa kirafiki dhidi ya Celtic, Tuchel alisema: "Yeye ni mchezaji wetu, ni nahodha wetu, na tunahitaji kuzungumza kuhusu hili baada ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.

"Leo ni muda wa kuangalia mbele. Inaonekana kama anaondoka, lakini kwenye soka huwezi kujua."

## ZISIKUPITE

### YAJITOSA KWA HANDERSON

CHELSEA inajiandaa kutoa ofa ya mshahara wa pauni 170,000 kwa wiki ili kujaribu kumshawishi golikipa wa Uingereza, Dean Henderson, 23, anayecheza kwa mkopo kule Sheffield United. ***(Manchester Evening News)***

### ANDRE TER STEGEN AWANIWA

KLABU ya Chelsea itajaribu kumsajili golikipa wa Barcelona na Ujerumani, Marc-Andre ter Stegen mwenye umri wa miaka 28, na wanajiandaa kumtoa Kepa Arrizabalaga mwenye umri wa miaka 25, kama sehemu ya dili hilo. ***(Mundo Deportivo)***

### YAKARIBIA KUMSAJILI TORRES

KLABU ya Manchester City inaonekana kuelekea kushinda mbio za kuwania kumsajili winga wa Valencia na Hispania, Ferran Torres. Borussia Dortmund pia imeonyesha nia ya kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 20. ***(Bild)***

### UTD, CHELSEA ZAMTAKA AKE

MANCHESTER United na Chelsea zimeungana na Manchester City kwenye mbio za kuwania kumsajili mlinzi wa Bournemouth na Uholanzi, Nathan Ake, 25. ***(Sun)***

### AUBAMEYANG KUBAKI ARSENAL

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta "anajiamini" mshambuliaji wa kimataifa wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 31, atasaini mkataba mpya na klabu hiyo. ***(Independent)***

### LEEDS UTD KUMSAJILI CAVANI

MMILIKI wa Leeds United, Andrea Radrizzani amesema "ataangalia" juu ya kumleta mshambuliaji Edinson Cavani mwenye umri wa miaka 33 raia wa Uruguay klabuni hapo baada ya timu hiyo kupanda kwenye Ligi Kuu ya England. Cavani anaondoka Paris St-Germain kipindi cha majira ya joto baada ya mkataba wake kumalizika. ***(Sky Sports Italia, via Football Italia)***

### PIERRE-EMILE ATUA EVERTON

KLABU ya Everton imefikia makubaliano binafsi na kiungo wa Southampton, Pierre-Emile Hojbjerg raia wa Denmark mwenye umri wa miaka 24, baada ya klabu yake kukubali ada ya pauni milioni 25. ***(Daily Echo)***

### WEST HAM KUMCHUKUA TOMAS

KLABU ya West Ham inaweza kuamua kumsajili kwa mkataba wa kudumu kiungo wa Jamhuri ya Czech, Tomas Soucek mwenye umri wa miaka 25 ambaye anacheza kwa mkopo hapo kutoka Slavia Prague kwa ada ya uhamisho ya pauni milioni 18.9, klabu hiyo ya Ligi Kuu ya England imethibitisha. ***(Telegraph)***

### MBWANA KWENDA FANERBAHCE

FOWADI wa Aston Villa na Taida Stars, Mbwana Samatta, 27, anaweza kwenda kwenye klabu ya Fenerbahce baada ya kushinda kuwa na kiwango cha kuvutia pale Villa Park, tangu alipotua Januari mwaka huu. ***(Takvim via Sport Witness)***

### AREOLA KUTUA EPL

GOLIKIPA wa Paris St-Germain, Alphonse Areola mwenye umri wa miaka 27, ambaye anacheza kwa mkopo pale Real Madrid, anaweza kwenda kwenye Ligi Kuu ya England baada ya nyota huyo wa kimataifa wa Ufaransa kununua nyumba jijini London. ***(Marca)***

## HABARI MICHEZO

# Ally Choki kuwasindikiza Waluguru Original

**Na Sabato Kasika**

MWANAMUZIKI maarufu nchini, Ally Choki anatarajia kusindikiza uzinduzi wa albamu mpya ya bendi ya muziki wa dansi ya Waluguru Original unaotarajiwa kufanyika Agosti 7, mwaka huu.

Choki, nyota wa zamani wa African Stars 'Twanga Pepeta' atapamba uzinduzi huo akiwa na bendi ya The Bambazi inayoongozwa na Mulemule FBI.

Mkurugenzi wa Waluguru Original, Killer Man, alisema maandalizi ya onyesho hilo yako katika hatua za mwisho na jina la albamu hiyo ya pili itakayozinduliwa ni Kikao cha Wahenga. Alizitaja nyimbo zinazounda albamu hiyo ni pamoja na Morogoro Yetu, Mwanzo wa Mapenzi, Cha Kupewa, Ngalile Mwanangu Ndole, Supu na Nataka Nilewe'.

"Kwa sasa tupo jijini Dar es Salaam tukimalizia kurekodi nyimbo zetu, ili siku ya uzinduzi tuwe na audio kwa ajili mashabiki watakaohitaji kuzinunua ili wazipate siku hiyo," alisema Killer Man.

Alisema wamemwalika Choki na Mulemule kwa sababu ni marafiki zao na wanafahamu watawapa burudani nzuri mashabiki wa muziki hapo Morogoro.

"Lakini napenda kuwaongezea mashabiki wetu, pamoja na kutusindikiza, Mulemule pia atazindua bendi yake kwenye onyesho hilo, ambalo litafanyika kwenye ukumbi wa Terminal Pub uliopo eneo la Msamvu," aliongeza.

# DAS Muheza aachia wimbo wa kampeni

**Na Steven William,** MUHEZA

KATIBU Tawala wa Wilaya ya Muheza Mkoa wa Tanga, Desderia Haule (DAS), ameachia wimbo wa kumuunga mkono Rais John Magufuli katika kampeni ya uchaguzi mkuu wa mwaka huu.

Wimbo huo umepewa jina la 'Amechaguliwa na Mungu kuwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.'

Desderia aliutambulisha wimbo huo katika ukumbi wa Tate Plus wakati wa upigaji kura ya maoni kuwapitisha wagombea ubunge wa Jimbo la Muheza kwa tiketi ya Chama Cha Mapinduzi CCM.

Wakati akiutambulisha wimbo huo, alisema ametunga wimbo huo kwa ajili ya kuwahamasiaha wananchi kumchagua kwa kishindo katika uchaguzi mkuu wa mwaka huu utakaofanyika Oktoba 28 mwaka huu.

Alisema kuwa wimbo huo wa hamasa wakati huu kuelekea uchaguzi mkuu ni zawadi yake maalum ya maneno kwa njia ya muziki kwa mgombea urais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania John Magufuli.

Alisema kuwa hivyo ameona atumie kipaji ayaweke baadhi ya maneno ya kabila la kwao la Kingoni, watu wa Songea katika albamu hiyo kwani ipo siku yatakuja kumfikia mgombea urais John Magufuli.

# GWAMBINA KUWAPOTEZEA WAKONGWE SIMBA, YANGA

**Na Saada Akida**

KATIKA kuimarisha kikosi chake kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Kocha Mkuu wa Gwambina FC, Novatus Fulgence, amesema anahitaji kusajili wachezaji wapya sita ambao watasaidia kuhimili changamoto za ligi hiyo ya juu nchini.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Fulgence alisema usajili huo utaangalia nafasi zote zenye mapungufu ikiwamo ya ushambuliaji, kiungo na ulinzi.**

Fulgence alisema anafahamu changamoto iliyoko kwenye Ligi Kuu na ili kufanya vema, atalazimika kusajili wachezaji watakaoongeza nguvu na vile vile kuifanya timu yake kuwa na kikosi kipana.

"Hatubomoi timu yetu ila tutaboresha kikosi chetu, tutayafanyia kazi mapungufu yaliyopo, lakini tuwe na kikosi kipana, maana Ligi Kuu ina changamoto na ushindani, pia kuna suala la mchezaji kuumia au kutumikia adhabu ya kadi," alisema Fulgence.

Aliongeza anahitaji kuwa tofauti na timu zinazopanda daraja na kukimbilia kusajili nyota wanaoachwa na timu kongwe za Simba, Yanga au Azam FC na badala yake ataangalia zaidi wachezaji wenye kiwango bora kutoka katika timu za madaraja ya chini.

"Kikosi chetu sio kibaya sana, kuna maboresho madogo, nimeangalia wachezaji wa chini kwa kuwa wanatapambana kutupatia matokeo mazuri kwa sababu wanatafuta nafasi ya kucheza timu kubwa," Fulgence alisema.

Kocha huyo alisema unaposajili wachezaji 'waliotemwa' na timu hizo, hushindwa kujituma na kuonekana hawana cha kupoteza.

"Wachezaji wangu nimewapa mapumziko ya wiki moja, watarejea mazoezini Agosti 4, mwaka huu kwa ajili ya kujiandaa na msimu mpya, tunajua tutakutana na ligi ya ushindani mkubwa.

"Awali uongozi walipanga timu iende Afrika Kusini au moja ya nchi za Kiarabu, ila kutokana na huu ugonjwa wa corona na mipaka kufungwa, hatutajua kama safari hiyo itakuwapo," alisema Fulgence.

Aliongeza kabla ya kuanza msimu mpya, timu yake imeshaanza maandalizi ya kusaka mechi za kirafiki na timu mbalimbali za hapa nchini ili kuwajenga wachezaji wake.

Alieleza pia anatarajia kukabidhi ripoti yake kwa uongozi wa timu hiyo na endapo watashindwa kusafiri nje ya nchi, watakwenda kuweka kambi nyumbani kwao Misungwi.

Gwambina na Dodoma FC, zimepanda daraja moja kwa moja huku timu nyingine zitajulikana baada ya kumalizika kwa mechi za mtoano baadaye wiki ijayo.




Mshindi wa bonasi ya Jackpot wiki hii, Zaituni Fikiri Rwambo akishikilia mfano wa hundi ya Sh. 9,085,392 baada ya kubashiri kwa usahihi mechi 11 kati ya 13 kwenye Jackpot ya SportPesa. **PICHA: SPORTPESA**

# *Polisi Tanzania kujadili usajili Jumapili*

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Polisi Tanzania unatarajia kufanya kikao maalumu Jumapili ili kujadili hatima ya wachezaji ambao itawasajili na itakaowaacha kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Bara, imefahamika.

Kocha Mkuu wa Polisi Tanzania, Malale Hamsini, aliliambia gazeti hili wanahitaji kufikia uamuzi wa nyota itakaokuwa nao kwa ajili ya msimu mpya kwa sababu ya kujenga kikosi imara.

Malale alisema kikosi chake kitakuwa na mabadiliko makubwa na hii imetokana na mapungufu aliyoyabaini msimu huu ambayo hataki yajirudie tena.

"Benchi zima la ufundi pamoja na viongozi wa timu tutakuwa na kikao maalumu Jumapili, lengo kuu ni kujadili aina ya wachezaji ambao tutawasajili kwa ajili ya kutupa nguvu msimu ujao, alisema Malale.

Alisema pia atakutana na kila mchezaji aliyemaliza mkataba kwa lengo la kufahamu mahitaji yao kabla ya kusaini makubaliano mengine mapya.

"Wapo wachezaji ambao mikataba yao inamalizika mwisho wa msimu na kuna baadhi ambao watakwenda kwenye timu nyingine, hili lazima nilijue kabla ya kuwasilisha ripoti na kuingia kwenye kikao," Malale alisema.

Kocha huyo alitamba anatarajia kuanza msimu ujao na nguvu mpya tofauti na hali ilivyokuwa kwenye msimu huu ambao ulikuwa na changamoto mbalimbali ikiwamo 'likizo ndefu' ya ugonjwa wa corona.

Alisema amejipanga kuhakikisha anamaliza msimu kwa ushindi bila kuwaogopa mabingwa, Simba ambao watawakaribisha hapo Jumapili kwenye Uwanja wa Ushirika Mjini Moshi.

Michezo
Alhamisi Julai 23, 2020
Nipashe



Mbappe: Nitabaki PSG
UKURASA 22

# Yanga SC yaielekeza Mtibwa shimoni

## ●●● Yaisubirisha hadi Jumapili kujua hatima yake, ngoma mbichi kwa Azam...

**Na Isaac Kijoti,** MOROGORO

SARE ya bao 1-1 iliyoipata Yanga dhidi ya Mtibwa Sugar katika mechi ya Ligi Kuu iliyopigwa Uwanja wa Jamhuri jana, imerejesha mbio mpya za kumaliza nafasi ya pili kwenye ligi hiyo huku 'Wakata Miwa' hao wakielekea shimoni.

**Matokeo hayo yanaifanya Mtibwa Sugar sasa kufikisha pointi 42 katika nafasi ya 14 huku Yanga ikifisha alama 69 tatu mbele ya Azam itakayoshuka dimbani ugenini leo dhidi ya Mbeya City.**

Ikumbukwe tayari Simba wameutwaa ubingwa wa ligi hiyo, hivyo vita kubwa ipo kwa timu zaidi ya sita ambazo zinakaza buti kuepuka kushuka daraja ama kuelekea kucheza mechi za mchujo.

Lakini pia kuna vita vingine kati ya Yanga na Azam kuwania heshima ya kumaliza nafasi ya pili wakati huu 'Wanalambalamba' hao wakitarajia kushuka katika Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya leo kuivaa Mbeya City katika mechi yao ya 37.

Hivyo, endapo Azam itashinda leo, itafikisha alama sawa na Yanga lakini itakaa juu kutokana na utajiri wa mabao, jambo ambalo litazilazimisha timu hizo kusubiri matokeo ya mechi zao za mwisho zitakapozivaa Tanzania Prisons na Lipuli FC ugenini kujua nani anamaliza nafasi ya pili.

Katika mechi ya jana, ilianza kwa kasi Yanga ikiwa ya kwanza kuliandama lango la Mtibwa na kupata kona doto dakika ya pili lakini ziligeuka kuwa tasa.

Dakika ya tano na saba Mtibwa iliiliandama lango la Yanga na kupata faulo mbili lakini hazikuwa na macho.

Salum Kihimbwa akiwa wingi wa kulia alitumia mabavu na ujanja dhidi ya Juma Makapu na kupiga krosi iliyounganishwa nyavuni na Haruna Chanongo dakika ya 28.

Mtibwa iliendelea kuliandama lango la Yanga ikiongozwa na Kihimbwa ambaye alionekana kuisumbua safu ya ulinzi ya iliyokuwa ikiongozwa na Lamine Moro, lakini dakika 45 za kipindi cha kwanza zikamalizika matokeo yakibaki kuwa 1-0.

Kipindi cha pili Yanga ilirejea bila Lamine ambaye aliumia dakika moja kabla ya mapumziko, hivyo nafasi yake kuchukuliwa na Bitriam Nchimbi.

Dakika ya 53 David Molinga akampisha Mrisho Ngasa huku dakika tano baadaye Jaffary Kibaya akikosa bao la wazi baada ya kutanguliziwa mpira mrefu akiwa amebaki na Kipa wa Yanga, Ramadhani Kabwili shuti lake likatoka nje.

Kocha wa Yanga, Luc Eymael, alionyesha anataka bao zaidi baada ya kumtoa kiungo Abduliaziz Makame dakika ya 78 na kumuingiza Tariq Self. Dakika tano baadaye, mpira wa adhabu ndogo uliopigwa pasi fupi ya haraka na Deus Kaseke ulizamishwa kimyani na Adeyun Saleh na kumwacha Kipa wa Mtibwa, Said Mohamed 'Nduda' akiwa hana la kufanya.

Zuber Katwila, Kocha Mkuu wa Mtibwa Sugar alimtoa Kibaya dakika ya 84 na kumuingiza Henry Sindika kuimarisha eneo la kiungo, lakini mabadiliko hayo hayakuweza kubadili matokeo.

Yanga ilicheza dakika tano pungufu baada ya Kaseke kuonyeshwa kadi ya pili ya njano ikiambatana na nyekundu.



Mshambuliaji wa Aston Villa, Mbwana Samatta, akipambana na mlinzi wa Arsenal, David Luiz wakati wa mchezo baina ya timu hizo kwenye Ligi Kuu ya England, juzi Jumanne usiku katika uwanja wa Villa Park mjini Birmingham, England. Aston Villa ilishinda bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Simba, Coastal ufundi kutawala

**Na Somoe Ng'itu,** TANGA

BURUDANI na soka la kiufundi linatarajiwa kuonekana katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara kati ya Coastal Union dhidi ya Simba itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa CCM Mkwakwani jijini, Tanga.

Mabingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu, Simba watashuka dimbani wakiwa na kumbukumbu ya ushindi wa mabao 2-0 waliopata katika mchezo wa mzunguko wa kwanza huku mechi iliyopita dhidi ya Alliance FC waliondoka na ushindi mnono wa magoli 5-1.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, ameliambia Nipashe kikosi chake kiko katika hali nzuri na wanahitaji kuendeleza kasi ya ushindi katika ligi hiyo ambayo sasa 'vita' yake imebakia kwa timu zinazopambana kujiepusha na janga la kushuka daraja.

Sven alisema hakuna mechi rahisi katika ligi hiyo ingawa leo anakutana na timu isiyokuwa na presha ya aina yoyote kwa sababu iko mahali salama.

Mbelgiji huyo alisema anahitaji kuona wachezaji wake wanajituma katika mchezo huo ili kuendelea kujiimarisha na kujiweka tayari na mechi ya fainali ya mashindano ya Kombe la FA inayowasubiri.

"Ni mechi itakayokuwa na burudani na mambo mengi ya kiufundi, kila timu itaingia uwanjani bila mawazo, sisi tayari ni mabingwa na wenzetu hawana cha kupoteza, wote tunahitaji heshima kwa mashabiki wetu pia, kila siku hakuna anayependa kuona timu yake inafungwa," alisema Sven.

Juma Mgunda, Kocha Mkuu wa Coastal Union alisema wamejipanga kusaka ushindi katika mechi ya leo na kumaliza 'uteja' dhidi ya mabingwa hao wa Bara.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >